**24 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 24 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 662

**Hitaji la Jengo la Mama na Mtoto, Kituo cha Afya Mkolani**

**MHE. MARY F. MASANJA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya Mkolani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mkolani kilipokea fedha, shilingi milioni 500,000,000.00 katika mwaka wa fedha 2023/2024, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)*, jengo la maabara, jengo la upasuaji na jengo la kichomea taka. Majengo yote haya yamekamilika na yanatoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali, kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, itatenga shilingi milioni 250,000,000.00, kwa ajili ujenzi wa jengo la huduma za baba, mama na mtoto pamoja na wodi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mary Francis Masanja, swali la nyongeza.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeweza kuboresha miundombinu ya afya katika Mkoa wa Mwanza. Miundombinu ya afya mingi imeboreshwa.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza. Pale wodi ya mama na mtoto pana changamoto, hawana mahali ambapo wanaweza wakajistiri. Ni lini Serikali itaweza kuanzisha miradi hii ili iweze kuwahudumia?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Pale kuna changamoto kidogo ya upungufu wa watumishi. Ni lini Serikali itaongeza watumishi katika Kituo cha Afya cha Mkolani, ili wananchi wanaozunguka eneo hilo waweze kupata huduma bora? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Mbunge wa Viti Maalum, kwa juhudi zake za mara kwa mara za kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Mwanza pamoja na wananchi wa Tanzania kwa ujumla. Hakika amekuwa anaifanya kazi hii kwa kufuatilia kwa karibu sana. Sisi tunamhakikishia kwamba, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kuhakikisha inatoa huduma hizo kwa kadiri ambavyo wananchi wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya cha Mkolani, tayari Serikali inaendelea. Hivi sasa ujenzi wa *walkway* na jengo la kufulia unaendelea katika Kituo cha Afya cha Mkolani.

Mheshimiwa Spika, pia mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma ya baba, mama na mtoto pamoja na wodi. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumeshaweka mpango kuhakikisha tunajenga majengo hayo mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi kuwa wachache. Ni kweli tunafahamu Kituo cha Afya cha Mkolani kinahudumia wananchi wengi, lakini Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kila mwaka wa fedha imeendelea kutoa ajira kwa watumishi wa kada mbalimbali za afya.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa jumla ya watumishi 34,720 wameajiriwa, lakini pia, Mkolani na Jiji la Mwanza wameendelea kupata watumishi. Kwa hiyo, nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jiji la Mwanza kwamba, Serikali itaendelea kupeleka watumishi ili kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Hai, wapo wagonjwa wengi wanaofika pale wenye matatizo ya

mifupa. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo la upasuaji, *theatre* ya mifupa katika hospitali ya Wilaya ya Hai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa miongozo yetu na Sera ya Wizara ya Afya, tuna huduma za afya za msingi, na pia tuna huduma za afya za rufaa. Halmashauri ya Wilaya ya Hai ina-*fall* katika eneo la huduma za afya ya msingi ambazo kwa sasa, kwa mujibu wa sera, hatuna madaktari bingwa wa mifupa kwenye ngazi za hospitali za halmashauri ambazo hazina hadhi ya mkoa au kanda au Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na utaratibu huo, hospitali nyingine za kanda, za rufaa na za Taifa zinatoa huduma hizo. Kwa mfano, kwa Kilimanjaro *KCMC* ni hospitali ya kanda ambayo inatoa huduma hizo, pamoja na pale *Mount Meru* na hospitali nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha tunaboresha huduma kwenye hospitali za rufaa, ili kwa wale ambao wanahitaji huduma za kibingwa za mifupa na huduma nyingine, wawe wanazipata karibu na maeneo yao katika mikoa hiyo wakati Serikali inaendelea kupitia taratibu na miongozo ya Sera za Afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kituo cha Afya cha Songwa katika Wilaya ya Kishapu, kuna tatizo kubwa sana la *walkway* kutoka kwenye jengo la akina mama, kiasi ambacho baada ya kujifungua inabidi wabebwe, ili kwenda kupelekwa wodini. Je, ni lini Serikali itasaidia miundombinu kwa ujumla katika kituo hiki kwa sababu zamani ilikuwa zahanati na sasa ni kituo cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Kituo cha Afya cha Songwa katika Jimbo la Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni moja ya vituo vya afya ambavyo vimepandishwa hadhi kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, amefika pale mara kadhaa na tumewasiliana na yeye na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwamba, wahakikishe wanatenga fedha za mapato ya ndani, kwa ajili ya ujenzi wa *walkway* hizo, ili akinamama wajawazito na wagonjwa wengine watumie *walkway* hizo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tulishakubaliana na tutakwenda kufuatilia. Nakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na Menejimenti ya Halmashauri ya Kishapu leo, ili kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Baada ya hapo, tutachukua hatua kuhakikisha kwamba, *walkway* hizo zinajengwa mapema iwezekanavyo.

**SPIKA.** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum. Swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Stella Fiyao.

Na. 663

**Kuajiri Wanasaikolojia Ngazi ya Kata**

**MHE. STELLA S. FIYAO k.n.y. MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri wanasaikolojia, ngazi ya kata, ili kusaidia kukabiliana na tatizo la afya ya akili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Muundo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Toleo la Mwaka 2022, huduma za kisaikolojia kwa watu wenye uhitaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hutolewa na Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe. Huduma hiyo hutolewa na Wataalam wa Kada ya Ustawi wa Jamii ambao hutekeleza jukumu hilo kupitia Makao Makuu ya Halmashauri na ngazi ya kata.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha utoaji wa huduma hiyo, Serikali imeajiri jumla ya wataalam wa kada ya ustawi wa jamii 1,546 na kuwapanga katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Serikali itaendelea kuajiri wataalamu wa Kada ya Ustawi wa Jamii na kuwapanga katika halmashauri zenye upungufu zaidi kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ukweli ni kwamba, changamoto ambayo inasababishwa na matatizo ya afya ya akili kwenye jamii zetu imekuwa ni kubwa sana. Tunaona vitendo vya ukatili, mauaji na mambo mbalimbali yanasababishwa na masuala ya afya ya akili.

Mheshimiwa Spika, je, hamuoni kuwa sasa ni wakati wa kuwahamasisha na kuwahimiza wataalam hao ambao wameajiriwa kwa kazi hiyo, kuwajibika ipasavyo kwenye jamii zetu, ili kuiepuka hii changamoto ambayo imekuwa ni kubwa na imekithiri sana kwenye jamii yetu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kumekuwa na ongezeko la changamoto ya afya ya akili na kuna uhitaji mkubwa wa wataalamu wetu kutoa huduma za afya ya akili, ustawi wa jamii na pia, huduma za kisaikolojia. Ndiyo maana Serikali imeendelea kuajiri wataalamu wa Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, wataalamu wote wa Sekta ya Afya; madaktari, wauguzi, Maafisa Ustawi wa Jamii na wengine, katika masomo yao wana *component* ya saikolojia ya binadamu *(Human Psychology)*. Kwa hiyo, tunaendelea kuhakikisha kwamba, katika vituo vyetu vya afya tunakuwa na wataalamu, madaktari na wauguzi ambao wana hiyo *component,* wanatoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, tunao Maafisa Ustawi wa Jamii katika ngazi ya halmashauri, katika vituo vya afya na hospitali, lakini pia, katika kata zetu tunaendelea kuwapeleka Maafisa Ustawi wa Jamii, ili kuhakikisha wananchi wote ambao wanahitaji huduma ya afya ya akili au ushauri na saikolojia, wanapata huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Fiyao kwamba, Serikali inaendelea kulifanyia kazi jambo hili. Tutaendelea kuboresha hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba, huduma zinawafikia vizuri zaidi wahitaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Hayupo, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, muulizie swali Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage.

Na. 664

**Kupandisha Madaraja ya Kiutumishi Madaktari Bingwa**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA K.n.y. MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuwapandisha madaraja ya kiutumishi madaktari bingwa bila sharti la ulazima wa kuandika andiko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Maendeleo ya Utumishi wa Kada ya Madaktari Bingwa unaotumika sasa, uliidhinishwa kupitia Waraka wa Maendeleo ya Utumishi, Na. 1 wa Mwaka 2009, ambapo sharti la machapisho liliwekwa kama la lazima kwa madaktari bingwa kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeandaa Rasimu ya Muundo wa Maendeleo ya Utumishi kwa kada zilizo chini ya Wizara ya Afya, ikiwemo kada ya madaktari bingwa. Katika rasimu hiyo, sharti la ulazima wa kuandika andiko kwa Madaktari Bingwa, ili kuwapandisha vyeo, limeondolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kuna uhitaji mkubwa sana wa madaktari bingwa katika *level* zote na wengi wameshajiendeleza, lakini suala la kigezo cha kuandika barua ya kupandishwa linakuwa ni kikwazo, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwapandisha hawa kwa sababu wanakuwa na kanzidata na wanawatambua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, Serikali iliona hivyo, ndiyo maana Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi, walikaa na kuondoa sharti hili la kuandika andiko, ili kupandishwa cheo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, hasa Mheshimiwa Dkt. Alice na Mheshimiwa Dkt. Christina kwamba, jambo hili tayari rasimu iko Ofisi ya Rais, Utumishi. Tutakapoanza mwaka wa fedha ujao, 2025/2026, hawa madaktari

bingwa ambao walikuwa na kikwazo kitakuwa kimeondoka, na kwamba, kwa nini tusiweze kuwapa mserereko?

Mheshimiwa Spika, hili jambo, kwa sababu muundo wa Mwaka 2009 ulikuwa hivyo, tutaanzia mwaka ujao wa fedha, hatuwezi kurudi nyuma. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha, 2025/2026, ndiyo tutaanza kutekeleza jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa jinsi ambavyo Serikali imekuwa sikivu mno kwa kilio cha madaktari bingwa ambao wanafanya kazi kubwa usiku na mchana, lakini ilikuwa mpaka wa-*publish* ndiyo wapandishwe daraja. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu na Serikali yake na sina swali la nyongeza. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 665

**Kukomesha Uzalishaji wa Mifuko ya *Plastic* Nchini**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakomesha kabisa uzalishaji, usambazaji na matumizi ya mifuko ya plastiki nchini?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha inakomesha uzalishaji, usambazaji na matumizi ya plastiki nchini. Hatua hizo ni pamoja na kupiga marufuku uingizaji nchini, uzalishaji, usambazaji, uhifadhi, usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019, kupitia Tangazo la Serikali, Na. 394, la Mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuandaa Kanuni za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za Mwaka 2019 kupitia Tangazo la Serikali, Na. 394, la Mwaka 2019, ambapo Mwaka 2022 kanuni hizo zilifanyiwa mapitio kwa kuongeza marufuku ya lakiri za vifuniko vya plastiki kwenye chupa za maji na vinywaji kupitia Tangazo la Serikali, Na. 291 la Mwaka 2022 na kuundwa kwa Kikosi Kazi cha Taifa ambacho kinaratibu utekelezaji wa katazo husika, kikijumuisha Wizara na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua dhidi ya wanaokiuka katazo hili, ikiwemo viongozi mbalimbali kutoa matamko, kwa ajili ya kusisitiza utekelezaji wa marufuku ya mifuko ya plastiki nchini, utoaji wa elimu kwa umma kuhusu vifungashio vya plastiki visivyoruhusiwa kisheria, utoaji wa adhabu kali kwa wazalishaji, wasambazaji, wauzaji na watumiaji wa vifungashio vya plastiki vilivyopigwa marufuku na kufanya kaguzi kwenye viwanda, maeneo ya biashara na mipaka ya nchi ambapo jumla ya viwanda 533 vya bidhaa za plastiki, wafanyabiashara 264 na Masoko 84 yamekaguliwa. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na Serikali, lakini bado inaonekana changamoto ipo. Je, Serikali haifikirii kuja na mpango mahsusi, ili kuzifanya taka hizo kuwa fursa kwa vijana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali ina mpango gani kuweza kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kujua na kutambua kwa kina vipi vifungashio vinavyoruhusiwa na vipi visivyoruhusiwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Zanzibar. Nachukua fursa hii kumpongeza sana kwa kuwa, amekuwa mdau mzuri sana wa mazingira na kutaka kujua baadhi ya mambo mengi kwa ajili ya uhifadhi na utunzaji.

Mheshimiwa Spika, upo ama ipo mipango mahsusi ambayo, kama Serikali tumeichukua kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na taasisi ikiwemo *NEMC* na nyinginezo kuhakikisha kwamba tunafanya taka zinakuwa fursa kwa vijana. Huko zamani taka zilikuwa ni uchafu, lakini sasa tumejitahidi kutoa elimu kwa vijana na Tanzania kwa ujumla ili waweze kujua kwamba taka ni fursa na zinaweza zikawanasua vijana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pia, tumeanzisha kituo maalum cha kuchakata taka, lengo na madhumuni ni vijana waende wakajifunze hapo na kuweza kupata taaluma. Tumekuwa tunaanza kutoa vibali *at least* vya kukusanya zile taka, hasa taka za plastiki.

Mheshimiwa Spika, ipo miongozo mbalimbali tumeianzisha ukiwepo mwongozo unaosema, "Punguza, Tumia Tena," kwa maana ya, "*Reduce, Re-use and Recycle*." Lengo ni chupa inayotupwa mtaani iweze kutumika tena baada ya kuchakatwa. Kwa hiyo, ziko hatua ambazo tumezifanya, na siyo taka za plastiki tu, taka nyingi tumekuwa tunazifanya zinakuwa fursa na zinaleta tija kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunatoa elimu kuwajulisha wananchi ili waweze kufahamu ni vipi vifungashio vilivyopo kisheria na vipi ambavyo havipo kisheria. Tumekuwa tunawaelemisha kupitia *task force* maalum iliyoundwa na *NEMC* kupitia kanda zetu maalum ambazo zipo nchi nzima. Huko nako tunatoa taaluma kuwaambia wananchi, vifungashio ambavyo vimeruhusiwa kisheria ni vile ambavyo vimethibitishwa kitaalamu, hasa kupitia *TBS* na vile ambavyo vitakuwa vina *contact* maalum, ili hata vikienea mtaani tujue nani tunamkamata? Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni lini *NEMC* itakuwa na mamlaka, ili ipate nguvu ya kupambana na kuenea kwa taka za plastiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunapata hayo masuala mara kwa mara kuulizwa kwamba lini *NEMC* itakuwa mamlaka, na ninadhani kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wameona kuwa kuna baadhi ya mambo labda yamekuwa hayaendi vizuri kwa sababu wanahisi *NEMC* bado haijakuwa mamlaka.

Mheshimiwa Spika, niwaambie tu kwamba, mchakato wa kuifanya *NEMC* kuwa na mamlaka, kuwa na nguvu za kuweza kufanya baadhi ya mambo na ikatekeleza, hususan ya ukusanyaji wa mapato na kuchukua hatua kwenye mambo kama haya, mchakato umeshaanza, na utakapokuwa tayari utaletwa Bungeni Waheshimiwa Wabunge wataujadili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sheria pamoja na kanuni kutungwa ni jambo moja, lakini usimamizi wa sheria ni jambo la pili, na ni muhimu. Katika vyombo vya baharini au katika vyombo vya maji ni sehemu kubwa ya kutumia kama ni dampo la kutupia takataka za plastiki, ikiwemo chupa na vifungashio vingine vya plastiki. Je, una ushauri gani wa kuweza kuwawekea angalizo wenye kumiliki vyombo hivyo vya bahari? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa kuna baadhi ya tabia za baadhi ya wananchi kutokuheshimu na kufuata

sheria, hasa sheria hizi za usimamizi wa mazingira, hasa kwenye hivyo vyombo vya usafiri, tumekuwa tukiona huko.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tumeanzisha kitengo maalumu cha mazingira, hasa maeneo ya bandari. Lengo ni kuona kwamba vyombo vyote vinavyosafiri kupitia majini, tunahakikisha vinakaguliwa kimazingira na kuhakikisha kwamba yeyote anayetupa taka au anayeharibu mazingira ya bahari na kwenye vyombo ambayo vinaweza kuathiri wengine anachukuliwa hatua kisheria.

Mheshimiwa Spika, hili tunaendelea kulisimamia na tutalisimamia. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 666

**Huduma za Afya kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, ni utaratibu upi unatumika kutoa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu wasio na uwezo kabla ya kuanza kutumika kwa bima ya afya kwa wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa wananchi wasio na uwezo wa kuchangia gharama za huduma za afya, ikiwa ni pamoja na wale walio katika makundi maalumu ya kijamii, mathalani

wazee walio na umri zaidi ya miaka 60 ambao hawana uwezo wa kipato, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, watoto walio katika mazingira hatarishi, wanawake wajawazito na watu wasiojiweza kiuchumi. Pia, wenye magonjwa sugu kama saratani, UKIMWI, kisukari, magonjwa ya moyo, pumu, *sickle cell*, kifua kikuu, ukoma na magonjwa ya akili.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Afya ya 2007, Serikali hutoa msamaha kwa gharama za uchangiaji huduma za afya kwa wananchi wote wasio na uwezo wakiwemo watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, na ninaomba niipongeze Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo imeendelea kuweka mipango mizuri na mikakati kwa kundi la watu wenye ulemavu na makundi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina swali la nyongeza isipokuwa nina ushauri. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, mambo yaliyozungumzwa kwenye jibu la msingi ni mazuri sana, lakini sasa kuwe kuna ufuatiliaji wa utekelezwaji wa haya ambayo yamezungumzwa kwenye jibu la msingi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu hakukuwa na swali, umepewa ushauri. Nadhani uupokee huo ushauri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninapokea ushauri.

**SPIKA:** Haya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Stella Ikupa kwa sababu kwa miaka yote aliyokaa hapa Bungeni, nikisoma makaratasi mengi kwenye Wizara ya Afya kwenye eneo la kusaidia walemavu na watu wenye uhitaji

maalumu, tunaona maandiko na tunaona mawazo makubwa na *impact* kubwa aliyoileta Mheshimiwa Stella Ikupa kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu, sasa aulize swali lake.

Na. 667

**Kuendeleza Zao la Karanga – Dodoma**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Zao la Karanga katika Mkoa wa Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza zao la karanga katika Mkoa wa Dodoma, mikakati mbalimbali imefanywa na Serikali, ikiwa ni pamoja na kusambaza kwa wakulima tani mbili za mbegu zilizothibitishwa daraja la kwanza, ambazo zilitumika kuzalisha mbegu za kuazimiwa ubora *(QDS)* kwa ajili ya wakulima wa Halmashauri za Mpwapwa, Bahi, Chamwino, na Kongwa.

Mheshimiwa Spika, pia, katika msimu wa 2024/2025 Serikali kupitia *TARI–Naliendele* ilitoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha karanga kwa wakulima 640 kupitia mashamba darasa 124 katika mikoa inayozalisha karanga ikiwemo Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2025/2026 Serikali imepanga kuzalisha na kusambaza tani 20.1 za mbegu bora na kutoa elimu ya

kanuni bora za kilimo cha karanga kwa wakulima wa mikoa inayozalisha karanga, ikiwemo wakulima 1,200 na maafisa ugani 300 wa Mkoa wa Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza: -

(i) Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuanzisha mashamba makubwa ili mbegu aina ya mangaka iweze kuzalishwa kwa ajili ya kuhudumia mikoa yote ambayo inazalisha karanga?

(ii) Je, Serikali ina mkakati wa kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya karanga ili kuweza kupata mafuta ambayo pia yatasaidia katika kupunguza nakisi ya mafuta nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Dodoma kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano katika kutumikia wananchi wa mkoa wake.

Mheshimiwa Spika, nimthibitishie tu kwamba, moja, tunajua umuhimu wa mbegu hii ya mangaka ambayo ameielezea hapa. Moja ya mpango tulionao ni kuongeza mashamba darasa yatakayotumika kuzalisha mbegu kutoka 37 yaliyoko sasa mpaka 50 katika Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, lipo katika mipango ya Serikali na tupo katika hatua ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa viwanda vya usindikaji, jambo hilo sisi kama Wizara tumeshalitolea maelekezo na sasa hivi tunatafuta wawekezaji kwa ajili ya kuweka viwanda kwa ajili ya usindikaji wa mafuta yanayotokana na karanga na vilevile alizeti, kwa sababu, mahitaji makubwa na mafuta ya kula nchini bado tunayahitaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua zao la karanga kule Nachingwea ambako kulikuwa kunaongoza kwa kulima karanga huko nyuma? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninampongeza vilevile Mheshimiwa Tecla Ungele ambaye amefanya kazi nzuri katika Bunge na katika mkoa wake. Nimthibitishie tu, katika mikoa ambayo ipo na ambayo tunakwenda kuongea kasi ya kugawa mbegu bora na kuongeza uzalishaji, ni pamoja na Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa hiyo, Nachingwea ni sehemu ya mkoa ambao sisi kama Serikali tumeupa kipaumbele.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 668

**Barabara ya Busimbe Senta – Kagemu – Kemebose Hadi Kyamunene**

**MHE. STEPHEN L. BYABATO** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Busimbe Senta – Kagemu – Kemebose hadi Kyamunene – Bukoba Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Busimbe Senta – Kagemu – Kemebose hadi Kyamunene, Bukoba Mjini yenye urefu wa kilometa 6.88 unatekelezwa kwa awamu kulingana na

upatikanaji wa fedha, kwa kuanza na sehemu ya Busimbe Senta – Kagemu Kituoni ambapo tayari mkataba wa ujenzi umesainiwa na taratibu za malipo ya awali kwa mkandarasi zinaendelea. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN L. BYABATO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninaishukuru Serikali kwa kuamua kuanza kujenga barabara hiyo. Tunayo taarifa kwamba mkandarasi anayeita *Kajuna Investment* ameshapewa mkataba, ataanza kujenga kwa meta 300. Kwa hiyo, naomba niwe na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali kupitia *TANROADS* itapokea na kufanyia kazi maombi yetu ya kuzi-*upgrade* barabara kuzitoa *TARURA* kuzipeleka *TANROADS*, zinazotoka *Lake Oil* kwenda Kyamunene, lakini pia kutoka Kagemu kituo cha afya kwenda Kemebose?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba tulishampa taarifa kuwa maombi hayo tumeshayapokea, na kwamba Wizara inafanyia tathmini ili kuona hizo barabara zinakidhi vigezo halafu ziweze kupandishwa hadhi na kuhudumiwa na *TANROADS*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMARI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliamua kutujengea kilometa mbili Makao Makuu, kilometa mbili kwa kiwango cha lami, makao makuu pale Karumwa na kutujengea kilometa moja na kutufungia taa zaidi ya robo tatu ya hiyo kilometa, je, ni lini sasa watakwenda kuendelea kuijenga ile kilometa moja iliyobaki na kuongezea zile taa robo tatu iliyobaki kwenye ile kilometa ya mwanzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, sijampata vizuri. Anaulizia taa ama kilometa za lami? Sijamwelewa vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, inaonekana umeuliza labda maswali mawili kwa wakati mmoja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, hapana, ni swali moja.

**SPIKA:** Uliza moja kwa sababu ni la nyongeza.

**MHE. HUSSEN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iliamua kutujengea kilometa mbili za kiwango cha lami Makao Makuu ya Karumwa, na kwa kuwa Serikali ilishatujengea kilometa moja, ile kilometa moja lini itaanza kujengwa iliyobakia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa vizuri, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba tunakamilisha hiyo kilometa moja kwenda kuwa tatu.

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa. Sasa ili uwe umejibu vizuri, maana umesema kama umemwelewa vizuri. Lazima uwe umemwelewa ili majibu unayompa yawe ya swali lake. Hebu fafanua, Mheshimiwa Naibu Waziri hajaelewa ni barabara gani unazungumzia?

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, naomba kurudia. Kwa kuwa Serikali iliamua kutujengea kilometa mbili za lami pale Makao Makuu Karumwa na kutujengea kilometa moja mpaka sasa

hivi, ninapenda kujua ile kilometa nyingine ya pili itaanza kujengwa lini?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri umemwelewa Mbunge?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimemwelewa vizuri.

**SPIKA:** Haya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakamilisha hizo kilometa mbili. Mpango ni kwamba baada ya kukamilisha katika makao makuu yote ya miji, tutaweka pia na taa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa Mbande, Kisewe, Msongola, juu ya mkandarasi wa barabara anayejenga katika barabara hiyo na kusuasua kwake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kusuasua kwa mkandarasi ilikuwa ni kwa sababu ameleta hati ya madai ya fedha. Hivi sasa tunaandaa malipo yake ili aweze kukamilisha kazi ambayo ilikuwa imebaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshakamilisha upembuzi na usanifu wa kina wa Barabara ya *KIA* – Mererani – Orkesumet kuelekea Kiteto, je, ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tukishafanya usanifu wa kina hatua inayofuata ni kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Ole-Sendeka kwamba, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuanze kuijenga hiyo barabara kwa awamu kulingana na fedha zitakazopatikana. Mpango huo upo kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalumu sasa aulize swali lake.

Na. 669

**Ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi utaanza, ikizingatiwa imeharibika na inachukua mzigo mkubwa wa makaa ya mawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ukarabati kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi yenye urefu wa kilometa 201 unatekelezwa na Serikali kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Ili kurahisisha utekelezaji, mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni kutoka Mtwara – Mingoyo kilometa 82.27, pamoja na upanuzi wa barabara kuwa njia nne katika Mji wa Mtwara yenye urefu wa kilometa 3.82. Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu hii yupo *site* na anafanya maandalizi kwa ajili ya kuanza kazi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu ya pili ya kutoka Mingoyo – Nanganga – Masasi kilometa 118.24, mkataba umesainiwa tarehe 29 Aprili mwaka huu na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwamba ujenzi utaanza muda wowote kuanzia sasa. Hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, Serikali haioni haja ya kumtaka mkandarasi anayetengeneza Barabara ya Mnivata – Tandahimba – Newala kurekebisha Barabara ya mchepuko kwa sababu imekuwa na adha kubwa kwa wasafiri?

(ii) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Daraja la Mto Lukuledi lililopo Ndomoni kuelekea Nachingwea kwa sababu limekuwa linaharibika wakati wote wa mvua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza la Barabara ya Mnivata – Tandahimba – Newala hadi Masasi kuhusu barabara za mchepuo ni suala tu la utekelezaji, kwa sababu mkandarasi ama wakandarasi hawa wawili wako *site*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mtwara kuhakikisha kwamba mvua imeshaisha, mkandarasi huyu ama wakandarasi hawa wawili waweze kuhakikisha kwamba wanatengeneza njia mbadala kwa maana ya mchepuko wakati zile barabara zinatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Daraja la Lukuledi, ni kweli tuna mpango wa kulijenga hili daraja kwa utaratibu wa fedha za mkopo nafuu wa *World Bank*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa daraja hili litajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chingulie, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGULIE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale tuliambiwa mkandarasi ameshapatikana kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 55. Je, ni lini mkandarasi atafika *site* kwa ajili ya kuanza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Masasi – Nachingwea – Liwale, kilometa 175, tutaanza kujenga kilometa 55 na tutaanza kutoka Liwale hadi Kiangara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tulishasaini mkataba na sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya kumlipa mkandarasi huyo fedha ya awali ili aweze kuanza kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 670

**Ujenzi wa Barabara ya Mlandizi – Ruvu *SGR* Stesheni**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mlandizi hadi Ruvu kwenye Stesheni ya *SGR?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imepanga kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa awamu ambapo mkataba wa ujenzi sehemu ya Mlandizi hadi makutano ya stesheni ya *SGR* na Ruvu, kilometa 15 imesainiwa tarehe 2 Mei, 2025, na mkandarasi yupo kwenye hatua za awali za kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sehemu ya Makutano ya Ruvu hadi stesheni ya *SGR*, kilometa nane, maandalizi ya usanifu

yanaendelea na kazi ya usanifu inategemewa kuchukua muda wa miezi mitatu. Baada ya usanifu kukamilika, zabuni za ujenzi zitatangazwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, na hapa ninapenda kutoa shukurani tu kwa Serikali kwa sababu majibu ya Serikali Wanakibaha wameyapokea kwa sababu ni kweli tarehe hiyo aliyoitaja mkandarasi amesaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sina swali isipokuwa ninaiomba Serikali, kutokana na kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa, basi iweze kufanya jitihada hasa kwenye wakati huu tulionao. Mkandarasi afike *site* mapema na aweze kufanya kazi na wananchi waone shughuli hiyo ikiendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninadhani umeshayapokea hayo maombi. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, tuna barabara kubwa ya lami ambayo kwa mujibu wa taratibu huwa mnaweka taa za barabarani. Katika Mji wa Namtumbo waliweka robo tu ya eneo taa za barabarani, lakini maeneo mengine makubwa waliacha hawakuweka watu wa *TANROADS*. Je, Serikali ipo tayari kuelekeza watu wa *TANROADS* mkoa wamalizie ile kazi ya uwekaji taa Mji wa Namtumbo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti tuliyoipanga kwa mwaka ambao tumepitishiwa, tuna sehemu kubwa sana ya kununua taa. Nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Ruvuma aweze kwenda Mji wa Namtumbo ili afanye tathmini na kuhakiki maeneo ambayo yanahitaji taa ili tupate mahitaji na tuweze kuweka

taa katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anakadiria ni muda gani utatumika kutoa fedha za kianzio kwa ajili ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara kutoka Rwanda mpaka Ndumbi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali hilo ni maalumu, kama unazo tarehe unaweza kumjibu; kama huna utazitafuta ili umpatie Mheshimiwa Mbunge, kanuni zinakuruhusu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo tumeshasaini na tunachosubiri ni kupata malipo ya awali ambapo wenzetu wa fedha; Wizara ya Fedha wameshatuahidi kwamba muda wowote barabara zote ambazo zimesainiwa watatoa fedha za malipo ya awali. Kinachosubiriwa ni malipo ya awali, Mkandarasi alishapatikana, tulishasaini mkataba, tunasubiri fedha ya awali kwa maana ya *advance payment*.

**SPIKA:** Sasa huo muda wowote ndiyo alikuwa anataka umwambie. Yaani swali lake lipo hapo kwenye muda ndiyo maana nikakwambia utampatia muda ama unao? Kwa sababu yeye kasema unakadiria vipi muda ambao fedha hizo zitatolewa, ndiyo swali lake.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, *okay*. Basi niseme tu tutaongea na wenzetu wa fedha tuone lini ili tumpe jibu sahihi lini tutamlipa Mkandarasi hiyo fedha ya awali ili aweze kuanza kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ipi kauli ya Serikali juu ya ukarabati wa barabara kuu inayotoka Singida – Babati hasa eneo la Gehandu – Dareda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ukarabati wa Barabara ya Singida – Babati pamoja na barabara nyingi ambazo zimechoka tumeziweka kwenye mpango. Katika mwaka unaokuja wa fedha Wizara imeamua kwamba itapeleka fedha nyingi sana kwenye ukarabati wa barabara nyingi ambazo zimechoka, ikiwepo Barabara ya Katesh kwenda Singida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 671

**Kuondoa Nyumba Zisizo na Ubora**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaondoa nyumba zisizo na ubora nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 Toleo la Mwaka 2023 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 zinahimiza uboreshaji wa makazi chakavu au yasiyopangwa katika maeneo ya miji kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma za miundombinu sambamba na kuongeza mchango wa maeneo hayo katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo hayo ya kisera, Serikali inaendelea kubadili taswira ya miji yetu kupitia miradi mbalimbali ya ujenzi inayotekelezwa na Shirika letu la Nyumba la Taifa *(National Housing Corporation)*, Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)*, *Watumishi Housing Investment* na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada hizo, hivi karibuni Wizara imeanzisha programu maalumu ya uendelezaji upya maeneo chakavu katika miji ambayo inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa huduma za msingi.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu hii, jumla ya maeneo 111 yenye ukubwa wa hekta 24,309.35 yameainishwa katika mikoa 24 kwa ajili ya uendelezaji upya ili yawe na tija kiuchumi na kijamii. Ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, kuwahimiza wananchi na wadau wengine katika maeneo yatakayoguswa na programu hii kutoa ushirikiano, hivyo kurahisisha zoezi la kuondoa makazi chakavu na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa kipato cha chini wanapata mkopo nafuu kwa ajili ya kujenga nyumba bora hasa vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Je, nini mkakati wa Serikali wa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu viwango sahihi vya ujenzi wa nyumba bora na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mikopo nafuu kimsingi benki zimeshirikishwa kwa karibu sana kujaribu kupunguza riba kubwa ambazo wanazitoza kwa ajili ya wakopaji wanaokwenda kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuhusu suala la elimu, tumeanza kutoa elimu juu ya nyumba bora ambazo wanastahili wananchi kujenga. Kimsingi ujenzi wa majengo haya unategemea vilevile uwezo binafsi wa wajenzi kwa kuzingatia uhalisia wa hali ya uchumi wao katika kuendesha, lakini tunatoa mwelekeo na elimu za kutosha kuhusu nyumba bora ziweje na ziwe na sifa gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia vyuo vikuu kuchora ramani rahisi na kuzigawa bure vijijini ili iwe kama walivyotoa zile ramani za vyoo wakati ule? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, kuhusu kuvitumia vyuo vyetu vikuu kwa ajili ya maboresho ya ramani za ujenzi wa nyumba zenye bei nafuu, lakini ameomba zitolewe bure. Sasa kwa sababu suala la uandaaji wa ramani linahitaji gharama, tulipokee tu hili jambo halafu tutakwenda kukutana na wenzetu aliowapendekeza tujaribu kuzungumza na kuona namna nzuri ya kutekeleza hili ambalo Mheshimiwa Dkt. Ntara, amelizungumza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 672

**Ongezeko la Idadi ya Wazee Nchini**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza: -

Je, Serikali inakabiliana vipi na ongezeko la idadi ya wazee katika nyanja za afya, lishe na huduma nyingine za msingi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ongezeko la idadi ya wazee ni kiashiria cha kuboreshwa na huduma mbalimbali kwa wazee ikiwa ni pamoja na huduma za afya, matunzo na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Tanzania ilikuwa na jumla ya watu 61,741,120. Kati yao, Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya wazee milioni 3.4; wanaume wakiwa na idadi ya milioni 1.5 na wanawake milioni 1.8 ikilinganishwa na mwaka 2012 ambapo idadi ya watu ilikuwa milioni 44.9; kati yao wazee walikuwa milioni 2.5 ambapo wanaume walikuwa milioni 1.2 na wanawake milioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, Wizara imehuisha Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 na kutoa toleo la mwaka 2024 ambalo limejielekeza kwenye kuboresha huduma za wazee kulingana na mahitaji ya wakati wa sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini kuna ongezeko la wazee ambapo kuna wazee ambao wana vitambulisho tayari ambao wanatakiwa kwenda hospitali na watibiwe bure. Pia kumekuwa kuna tatizo kubwa kwamba hao wazee wana vitambulisho, lakini bado hawawezi kupata matibabu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali inajua kwamba kwa sasa wazee wameongezeka, Serikali ina mpango gani

kuhakikisha inaleta programu maalumu ambayo itawasaidia wazee ili waweze kujua ni chakula gani wanaweza wakala ili waweze kuepukana na magojwa na mambo mengine kama hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa mwaka 2024/2025 imewatambua wazee 4,975,473 kwa mikoa yote ya Tanzania na Serikali imethibitisha wazee 2,199,588 hawana uwezo wa matibabu na imewapatia bima za afya ambazo zimeboreshwa kwa ajili ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, pia, katika hospitali zetu zote za mikoa tumeweka madirisha maalumu kwa ajili ya kuwasaidia wazee ambayo yanasema "Mpishe Mzee Kwanza." Ninawaomba tu wahudumu wa afya mikoa yote, sehemu zote, kuhakikisha yale madirisha wanayatumia vilivyo kama tulivyoelekeza ili wazee hawa wasipate shida katika kupata matibabu yao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya Awamu ya Sita, imeweka utaratibu maalumu wa kuwapa lishe wazee. Katika mikoa yetu yote Mheshimiwa Rais anatoa fedha shilingi milioni 118 kwa kila mwezi kwa ajili ya huduma mbalimbali za wazee ikiwemo lishe. Aidha, katika makazi yetu ya wazee tunao Maafisa Lishe ambao wanawapa utaratibu mzuri wa vyakula ili wazee hawa wawe na afya njema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 673

**Miradi Mikubwa ya Maji Kwenye Miji ya Jimbo la Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka miradi mikubwa ya maji kwenye Miji Midogo ya Mlangali, Lugarawa na Luilo ili kuendana na kasi ya ongezeko la watu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji wa Lifua - Manda unaohudumia vijiji vya Luilo, Lihagule, Kingole na Nsungu ambapo ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 75,000 unaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Miji Midogo ya Mlangali, Lugarawa na Luilo, Serikali inaendelea na ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 500,000 katika Mji Mdogo wa Mlangali kupitia Mkandarasi atayetekeleza ujenzi wa mradi wa barabara ya zege kutoka Itoni kwenda Manda kama sehemu ya kurejesha kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miundombinu ya usambazaji wa maji kutoka eneo la tanki la maji lenye ujazo wa lita 500,000 kwenda katika vijiji vya Mlangali na Itundu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Niitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali, kwani miaka hii mitano ambayo nimekuwa Mbunge, nimeshuhudia fedha nyingi sana ambazo zimeingia kwa ajili ya miradi ya maji Ludewa. Kwa

hiyo, ninaishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu zile changamoto chache ambazo wananchi bado wanalalamikia Mawengi, Igalu, Ligumbilo na maeneo mengine (niliziandika vizuri) nitaweza kumkabidhi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninadhani halikuwa swali, kwa hiyo, upokee hizo sifa kwa sekunde 30.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, na ninamshukuru sana kaka yangu, maana yake ameona Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya kazi kubwa sana, na katika maeneo ambayo yamebaki na changamoto hizo, Serikali ipo tayari kuzipokea na kuzifanyia kazi kwa niaba ya wananchi wake wa Ludewa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri Aweso waliniahidi kwamba wataenda kwenye kata zangu za Pemba na Mbogi kuangalia uwezekano wa kupata chanzo cha maji watu wangu wapate majisafi na salama. Je, lini watapeleka wataalamu pale watafute chanzo cha maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ili swali lako liweze kujibiwa na Naibu Waziri, sehemu ya kwanza umesema uliahidiwa na Waziri na Naibu Waziri kuwa watakuja. Sehemu ya pili, unasema lini watatuma wataalamu? Sasa chagua kimoja kati ya hapo ili nimwongoze Mheshimiwa Naibu Waziri ili aweze kukujibu sawa sawa. *(Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, wote wawili walishaahidi kupeleka wataalamu pale, hawajapeleka. Lini watawapeleka wataalamu hao ili watafute chanzo cha maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Waitara. Ni kweli kabisa Serikali ilishapokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge na kwa sababu tulikuwa katika Bunge lako hili, ninaamini kwamba tutatuma wataalamu wataenda, na baadaye watatupa mrejesho na tutachukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kwamba wananchi wa Mheshimiwa Waitara, wapate huduma ya majisafi na salama na hilo ndilo lengo kuu la Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kidogo tunaendelea kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga miradi ya maji katika Vijiji vya Kwiboa na Nansirori katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu kwa kuendelea kuwapigania wananchi wake wa Mwibara, na hakika kazi kubwa sana imefanyika kwa kushirikiana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hasa sisi Wizara ya Maji tunaendelea kuhakikisha kwamba utekelezaji wa ilani tunaufanya kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepitishiwa bajeti ya shilingi trilioni 1.061 kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba vijiji vingi vya nchini kote yanafanyiwa huduma ambayo itawafikia wananchi ikiwemo Jimbo la Mwibara. Kwa hiyo, nimtoe hofu, baada ya mwaka wa fedha kuanza, basi hatua stahiki zitaanza kuchukuliwa kwa ajili ya kufikisha huduma ya majisafi na salama. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, je, lini wananchi wa Kata ya Mahenge iliyopo katika Wilaya ya Kilolo watapatiwa mradi wa maji au japo kuchimbiwa kisima kwa sababu wamekuwa wakipata shida sana? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwa wananchi...

**SPIKA:** Hebu subiri Mheshimiwa Naibu Waziri, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, mnajadiliana mambo ya msingi sana, lakini punguzeni sauti. Hilo ni moja.

La pili, wale mnaoongea na simu, mnaanza kuongea kidogo kidogo, baadaye sauti zinapanda; ninadhani Wajumbe sijui, wanawasumbua huko! Sasa Waheshimiwa Wabunge, ambao ni lazima mzungumze na simu, basi unaweza kwenda nje ili ukitiwa hasira zile, upandishie ukiwa nje kuliko humu ndani, lakini wakati huohuo tupunguze basi sauti kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti. Najua tunajadiliana mambo ya muhimu, lakini tupunguze sauti kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na ninampongeza kwa kuendelea kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Iringa na kwa Eneo la Kilolo ambalo kata ile aliyoitaja inatoka katika Jimbo la Kilolo.

Mheshimiwa Spika, tutatuma wataalamu wetu kwenda kufanya tathmini na kujiridhisha hali halisi ya upatikanaji wa maji na baada ya hapo Serikali itachukua hatua stahiki ya kuwafikishia huduma ya majisafi na salama. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa maji katika Kijiji cha Wila na Kata ya Idukilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Butondo na kwa kazi kubwa sana ambayo anaendelea kuifanya katika Jimbo lake la Kishapu. Ameendelea kuwa sauti ya Wanakishapu kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la Wila, lipo katika utekelezaji wa miradi ya *P4R*, ambapo inatarajiwa kuanza mwezi wa Saba ambapo tunaamini kwamba mradi huu utakimbizwa haraka kulingana na kwamba mahitaji ya wananchi katika eneo hilo ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira kidogo, utekelezaji utaanza mwezi wa Saba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kata ya Buganguzi kwenye Jimbo langu la Muleba Kusini, tulibahatika kupata mradi mkubwa wa maji ulioenda kama 99%, lakini Umekwama kidogo. Je, ni nini kauli ya Serikali ili wananchi wale wapate maji salama katika huo mradi ambao Mama Samia alitupatia fedha nyingi, lakini umebaki kidogo tu? Nini kauli ya Serikali ili wananchi wapate maji hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sijalisikia vizuri swali.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Buganguzi Wilaya ya Muleba tunao mradi mkubwa wa maji ambao tumepata shilingi bilioni tatu, lakini unasuasua kidogo, tumefikia hatua ya 99%, imebaki kidogo tu kwa madai ya mkandarasi. Naomba kauli ya Serikali juu ya umaliziaji wa huo mradi wa maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu Mbunge wa Muleba Kusini.

Mheshimiwa Spika, mradi ukishafikia 99%, ni sawa sawa na kwamba mradi umeshakamilika. Kuna baadhi ya vitu vidogo vidogo ambavyo vitakuwa vinasubiriwa kukamilishwa ili uanze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji, kumwelekeza *RM* Mkoa wa Kagera kuhakikisha kwamba anaenda na kupata taarifa na atufikishie Wizarani ili tuone ni wapi palipokwama kuukamilisha mradi huo? Lengo ni kwamba wananchi wa Muleba Kusini ambao Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiwapambania sana, wapate huduma ya majisafi na salama kutokana na mradi huo ambao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliridhia kutoa zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta Subira, tutalifanyia kazi na tutampatia majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Eric Shigongo.

No. 674

**Mradi wa Maji wa Munyu - Singida Magharibi**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO K.n.y. MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Munyu katika Kata ya Irisya Jimbo la Singida Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa maji Munyu uliopo Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida na umeanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wapatao 2,199 wa Kijiji cha Munyu kinachopatikana katika Kata ya Irisya.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa tanki moja lenye ujazo wa lita 50,000, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house)*, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa nane, sanjari na ujenzi wa vituo vitano vya kuchotea maji. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Sasa liko swali la nyongeza moja tu. Mji wa Nyehunge kule Sengerema, Buchosa una matatizo makubwa sana ya maji. Upo mradi wa shilingi bilioni 40 ambao umekuwa-*designed* na Serikali. Je, Serikali itautekeleza mradi huo katika mwaka ujao wa fedha? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana namshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa na msemaji wa Buchosa au kisemeo cha wananchi wa

Buchosa. Natambua kabisa kwamba mradi huu ndiyo tegemeo la Mheshimiwa Mbunge la kutatua changamoto ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, naomba niliopokee nikaangalie kwenye *status* ya mradi huu imefikia wapi, kisha nitamjulisha Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wake wa Buchosa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wilaya ya Kilindi inategemea…

**SPIKA:** Subiri kwanza nikuite vizuri, maana niliona umeketi nikafikiri majibu labda yameshakuridhisha.

Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilindi inategemea mradi wa maji kutoka Kwedibuluma – Mvomero, Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya mahitaji ya Kata Nane, lakini leo ni mwaka wa tatu mradi huo unasuasua, haujaanza. Je, ni nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba mradi huo unaanza ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Kilindi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge. Mradi huu unaanza katika mwaka wa fedha ujao ambapo Mheshimiwa Mbunge ameshiriki katika kupitisha bajeti ya Serikali ya Wizara ya Maji. Lengo lake ni kwenda kuhakikisha miradi hii ambayo ilikuwa haijatolewa ile *advance payment* na wakandarasi wakashindwa kuingia kwenye utekelezaji, nimtoe hofu, mwaka wa fedha ujao mradi huu unaenda kuanza bila kuwa na shida yoyote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, Tunduru Mjini kuna changamoto kubwa sana ya maji na tunaishukuru Serikali mkandarasi tayari alishapatikana kutekeleza mradi ule wa maji Tunduru Mjini, lakini bado hajalipwa malipo ya awali ili aweze kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kufahamu, je, ni lini Serikali italipa malipo ya awali ili mkandarasi yule aanze kazi na kumaliza tatizo la maji Tunduru Mjini? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu na pia tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi ndani ya Tunduru Mjini. Tayari Wizara ilishamwomba kukamilisha baadhi ya vipengele mkandarasi ili alete, na sisi tuwasilishe Wizara ya Fedha kwa ajili ya malipo, na baada ya hapo, mkandarasi ataingia *site* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inasikiliza wawakilishi wa wananchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujua katika Kata ya Mbanja Jimbo la Lindi Mjini, Kata ambayo unaenda kutekelezwa mradi mkubwa wa *LNG* hawapati majisafi na salama. Ni lini Serikali mtafanya maamuzi ya makusudi sasa ya kuleta fedha kwa ajili ya uwekezaji huo ili wananchi waweze kupata majisafi na salama? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, na pia ninamshukuru sana dada yangu kwa kuendelea kutekeleza

falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani kwa kuendelea kuwasemea wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara itatuma timu ya wataalam wakafanye tathmini na baada ya kufanya tathmini, basi tutajua ukubwa wa tatizo na baadaye Serikali itachukua hatua stahiki za kuwafikishia wananchi wa Mheshimiwa Mbunge majisafi na salama na yenye kutosheleza. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali.

Kule nyuma kuna Wabunge wamesimama, na mwingine anazungumza. Tafuta kiti uketi. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni asubuhi hii na tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wageni 45, hawa ni Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Kariakoo kutoka Wilaya na Mikoa mbalimbali ya Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, hawa ni Dkt. Fred Msemwa ambaye ni Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; yupo Dkt. Blandina Kilama, Naibu Katibu Mkuu Mtendaji, Mipango na Ubunifu. Ahsante sana.

Pia yupo Dkt. Mulisali Milanzi, Naibu Katibu Mtendaji, Mipango ya Kitaifa. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, huyu ni Ndugu Nasra Mohamed, Mwenyekiti wa UVCCM kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara. Hawa ni walimu wa Shule ya Sekondari ya Jokate kutoka Kisarawe Mkoani Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, hawa ni Wanawake Viongozi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Watendaji wa Kata na Vijiji kutoka Babati Mkoani Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 59 wa Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, ambao ni Walimu Wakuu kutoka Sumbawanga Mjini, Mkoani Rukwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Agnes Hokororo, ambaye ni dada yake kutoka Mkoani Morogoro, Ndugu Magreth Mpanda. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, ambao ni watoto wake kutoka Nachingwea Mkoani Lindi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, ambao wanatoka Chunya. Hawa ni marafiki zake kutoka Mkoani Mbeya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, ambaye ni Dkt. Mohamed Khalifa. Huyu ni mtoto wake kutoka Newala Mkoani Lindi. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma. Haya, karibuni sana. Angalau huyu namjua jina anaitwa Atika. Haya, hebu Atika simama.

Haya, yule pale juu jamani, huyo mtoto wa Mheshimiwa Lucy Mayenga. Ahsante sana. Niliwaambia jana changamoto yetu, lakini huyo ni mtoto wa Mheshimiwa Lucy Mayenga, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, ambao ni viongozi wa Chama na Serikali kutoka Songosongo, Kilwa, Mkoani Lindi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa na Sekretarieti ya CCM ya Wilaya ya Malinyi, Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni Sita wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ambao ni Viongozi wa Umoja wa Wazee kutoka Nyang'hwale, Mkoani Geita. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa, kutoka Wilaya ya Hanang' Mkoani Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni Tisa wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, ambao ni ndugu zake kutoka Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Iringa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 43 na walimu watano wa Shule ya Msingi *Trust St. Patrick* kutoka Sakina Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 55 na walimu wanne kutoka Shule ya Msingi *New Wisdom* ya Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wanawake 10 wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Mwenge Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao hapa Bungeni. Wengine tutaendelea kuwatangaza kadri wanavyopata nafasi ya kuingia hapa ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Tarimba Abbas, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuhusu Shindano la Taifa la Mpira wa Kikapu lijulikanalo kama *Taifa Cup 2025*.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa shindano la mpira wa kikapu lijulikanalo kama *Taifa Cup 2025* linaloshirikisha Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani, linalodhaminiwa na Benki ya *CRDB* na *Azam Media* linatarajiwa kuanza leo tarehe 24 Juni, hadi tarehe 04 Julai, katika Viwanja vya Chinangali, Dodoma. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria ikiwa ni pamoja na kuona timu zetu za mikoa zinavyoshinda katika shindano hili.

Waheshimiwa Wabunge, haya, kwa hiyo, mnakabirishwa huko Waheshimiwa Wabunge, lakini mkumbuke tu hii tarehe leo ni siku ya kura, sasa usije ukasema nilienda kuonana huko na watu wengine. Kwa hiyo, tukimaliza hapa, mnaweza kwenda huko, lakini mashindano haya yanaanza leo mpaka tarehe 04. Kwa hiyo, mtaweza kwenda siku nyingine pia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 76. Kwa sababu ya muda, naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Bunda makundi makubwa ya mnyama tembo yamevamia wananchi. Yamevamia vijiji 15 na mpaka leo saa mbili asubuhi makundi hayo yalikuwa bado yako kwenye maeneo hayo, wanakula mazao ya mashambani, wanakula

mazao kwenye maghala wanatishia wananchi kuamka usiku hata kutokutoka nje. Wanafanya kero kubwa sana kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninataka nipate mwongozo wako kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuyafukuza haya makundi ambayo yanatishia maisha ya wananchi kwenye Jimbo la Bunda? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kidogo. Nimesimama tena. Kule nyuma, bado mmesimama, mketi. Mtafute mahali pa kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, akiomba mwongozo kupitia Kanuni ya 76 kwamba kuna jambo ambalo limetokea huko Jimboni kwake, wananchi wamepata na wanaendelea kupata athari za uvamizi wa tembo katika maeneo yao.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Kanuni ya 76, kwanza haiwezi kutumika kwenye mazingira hayo kwa sababu Kanuni ya 76 inazungumzia jambo ambalo limetokea mapema hapa Bungeni na likitaka mwongozo kujua kama hilo jambo linaruhusiwa ama halirusiwi ili Kiti kitoe mwongozo.

Hoja aliyoisema Mheshimiwa Getere ya kwamba kuna athari huko ambazo wananchi wanazipata. Hata hivyo, hapa wakati wa kuzungumzia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, walizungumza mipango ya Serikali ya kununua ndege nyuki ya kuweka mazingira ambayo hakutakuwa na huo uvamizi katika maeneo ya wananchi ikiwa ni pamoja na kuchimba mabwawa kwenye maeneo ambayo yana wanyama ambao wanaweza kuvamia maeneo ya wananchi. *(Makofi)*

Sasa naona hapo Mheshimiwa Getere upo karibu kabisa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu jambo hili limeombwa kwenye mwongozo, hebu nenda hapo nyuma ukae na huyo Mheshimiwa Mbunge umweleweshe hoja huko

itakuwaje kwa wananchi? Kwa sababu athari zinaendelea mpaka sasa.

Nimesema hivyo kwa sababu amesema wananchi wamepata athari, lakini pia zinaendelea. Kwa hiyo, lazima suluhu itoke kwa namna ambayo jambo hilo linafika mwisho. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali kaa na Mheshimiwa Getere hapo, tena ikiwezekana mtoke nje kabisa maana inawezekana kuna kupiga simu ili hatua ziweze kuchukuliwa. Kwa hiyo, mnaweza kwenda nje kidogo mkazungumze hapo.

Kama Mheshimiwa Getere utakuwa hujapata majibu, sasa utarejea, lakini na Kanuni nyingine siyo Kanuni ya 76, unaweza kuleta hoja yako chini ya Kanuni nyingine inayohusu hoja ya dharura. Nendeni kwanza nje mkaongee, kama hayakwisha utarejea hapa ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI.

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026
### na
### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Sasa ninayo orodha hapa ya wachangiaji, lakini baada ya hao wachangiaji tutatoa fursa kwa watoa hoja kuhitimisha hoja zao.

Tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo.

Waheshimiwa Wabunge, niwaombe tena kwa sababu mnayo hiyo ruhusa, tupunguze sauti ili tuweze kusikia michango inayotolewa na wenzetu. Tupunguze sauti. Kama ni lazima kuwa na kikao kidogo mnaruhusiwa kwenda nje; na wale wa simu niwakumbushe tena, narudiarudia na bado ninawaona wanazungumza na simu.

Sasa mtaniwia radhi tuko mwishoni mwishoni kidogo, lakini nitawajulisha fulani nenda kaongee na simu nje kama huyu ninayemwona hapa. Ama niwaelekeze wazee wa kamera waanze kuwalekeza ili ukishajiona ndio utoke nje? Tupunguze sauti, tusikilizane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai, na leo tuko hapa tukiwa tunajadili suala ambalo ni suala la msingi kabisa katika Taifa letu, kwa maana ya kujadili mipango ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kushukuru na ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kabisa kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji katika kumsaidia Mheshimiwa Prof.Kitila Mkumbo katika jukumu kubwa katika ofisi hii kuhakikisha kwamba shughuli zote za uwekezaji na mipango ya nchi hii inakwenda kama ilivyostahili.

Mheshimiwa Spika, niendelee kukupongeza wewe, maana ninakumbuka kabla sijapata nafasi hii ya kuteuliwa, nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati. Tumefanya kazi pamoja, na kwa kweli wewe umekuwa mwalimu wangu mkubwa, umekuwa mwalimu mzuri unayeweza kufundisha mtu yeyote namna ya uongozi unavyotakiwa kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kazi yako iliyotukuka na kwa kweli Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki katika kazi zako, katika shughuli zako na hasa ile nafasi nyingine ya Urais wa Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru wewe pia pamoja na Naibu Spika ambaye ni Mheshimiwa Zungu. Kwa kweli naye pia amekuwa ni kiongozi mwema na kila mtu anapomwona Mheshimiwa Zungu anamfurahia kwa sababu amekuwa ni Naibu Spika ambaye kwa kweli tunampongeza kwa kazi yake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza Wenyeviti wote wa Bunge wanaokusaidia na Wenyeviti wote wa Kamati zote za Bunge. Kwa kweli tumefanya kazi kwa ushirikiano na hasa zile Kamati ambazo zinatusimamia ikiwemo Kamati ya Mitaji ya Umma na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Oran Njeza. Kwa kweli wamekuwa wakituelekeza vizuri na kwa kweli tumepata ushirikiano mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Waziri wangu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Profesa huyu amekuwa kwangu ni mwalimu mzuri na kwa kweli ninampongeza. Ninajisikia vizuri kufanya kazi naye kwa sababu amekuwa kwanza ana ukarimu wa kutosha, ni mwalimu mzuri, ni mbunifu, ni mvumilivu, na mwaminifu kwa Taifa lake.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tunaomba wananchi wa Jimbo la Ubungo waendelee kumwamini, na tunaomba sana wamrudishe Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kwa sababu Taifa linamtegemea. Taifa hili kwa kweli linategemea kichwa kama cha Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo kuweza kupata maendeleo ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na kwa kweli tumeshiriki kwa pamoja. Kama tunavyofahamu, Wizara hizi ni Wizara pacha, tumeshirikiana usiku na mchana, bega kwa bega. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tunaweza kusema ni mtu ambaye amebobea na

nafasi hii imemfaa na wananchi wa kule Iramba tunawaomba sana waturudishie Waziri huyu bila mashaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Naibu wake Mheshimiwa Chande ninampongeza. Nichukue fursa hii kumpongeza kwa kuteuliwa na yeye kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu na sasa ni Waziri ambaye yuko Kamati Kuu. Wananchi wa kule jimboni kwake ninadhani hawana haja ya kubadilisha Mbunge, kwani wanaye Mbunge wa kutosha na kwa kweli tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara yetu ilitoa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2024 na vilevile ikatoa Taarifa ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026. Katika hali ya uchumi nichukue fursa hii kabisa kabisa kumpongeza Rais wetu, maana hali ya uchumi wa nchi yetu imezidi kuimarika.

Mheshimiwa Spika, wakati huu tukiangalia katika nchi jirani au nchi za Kimataifa kwa maana kwamba nchi nyingine tumeona uchumi unavyotetereka, lakini kwa Tanzania tumeona kabisa uchumi wetu umezidi kuimarika na umekua kwa 5.1% kwa mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne ya Rais wetu na kukua huku kwa uchumi tunaona kabisa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweza kuwa ni kiongozi mzuri kwa sababu uongozi wake umekuwa mahiri, umekuwa thabiti, ana uvumilivu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia amekuwa ni mtu wa kutoa matumaini kwa watu wake au wananchi anaowaongoza. Uongozi wake umekuwa ni wa kujali wanyonge, umekuwa ni uongozi unaosikiliza, kuheshimu na kusimamia mawazo ya wananchi na haki za wananchi au haki za watu anaowaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu umezidi kuimarika. Hii ni kutokana na mipango ya maendeleo ambayo tunatambua kuwa ni nyenzo muhimu sana ya utekelezaji wa Ilani ya chama chetu cha Mapinduzi. Vilevile, mipango imekuwa ikizingatia Dira ya Taifa ya

Mwaka 2025, na sasa hivi tunakwenda kwenye Dira mpya ya mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, pia maandalizi ya Dira ya mwaka 2050 nayo yamezidi kuwa ni kichocheo na ni mtazamo ambao unaonekana kabisa mwelekeo wa uchumi unakwenda kuimaraika kwa maana ya maandalizi ya mpango yamekuwa thabiti na ni mazuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile taarifa yetu nyingine ilikuwa ni ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025/2026. Kwa kweli mpango huu ni Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano ambapo Mheshimiwa Waziri atakuja kueleza kwa undani zaidi. Hata hivyo, tumeona kabisa kwamba mpango huu wa maendeleo umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 na mikakati mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, tumeona Mawaziri pamoja na Wabunge wametoa michango mizuri sana ambayo kwa kweli mingi tumeipokea na kwa kweli wameonesha weledi wa hali ya juu katika kutoa ushauri wao na kuweza kuona kwamba kila sekta ni jambo gani tufanye ili tuweze kuimaraisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile mpango huu umezingatia Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Kusini mwa Afrika ya mwaka 2050 pamoja na ajenda ya mwaka 2063 ya maendeleo ya Afrika na malengo endelevu ya mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, haya yote, tukizingatia kwamba bajeti hii pamoja na mpango huu ni wa mwisho kwa ile Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na wakati huo huo tunajiandaa kwa Dira ya Mwaka 2050, tunaona kabisa Rais wetu amekuwa na maono ya hali ya juu. Ile Dira ya Mwaka 2025 tumeweza kuona mambo mengi yametekelezwa na mambo mengi yamezingatiwa katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mambo haya ambayo yameimarishwa, yatakwenda kutusaidia hata kwenda kutekeleza ile Dira ya Mwaka 2050 kwa kuzingatia kwamba kuna sekta ambazo tumeziona ni sekta

chochezi za uchumi ambazo Mheshimiwa Rais na Serikali yetu imezingatia kuona ni namna gani tunawekeza kule ili uchumi wetu uweze kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya sekta hizo tukitazama Sekta ya Miundombinu ambayo tunasema ni *enabling sector* ambayo inakwenda ku-*boost* uchumi wa nchi yetu, ukiangalia kwa upande wa miundombinu, Rais amefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, tumepeleka umeme vijiji vyote zaidi ya vijiji 12,300 na ushee na vijiji vyote vimeunganishiwa umeme. Pia, tukitazama uzalishaji wa umeme, uzinduzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na vyanzo vingine vya umeme tunatambua kabisa kwamba nishati ni kitu muhimu katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, ukitazama upande wa barabara tunaona mikoa yote imeunganishwa kwa kiwango cha lami. Pia, tunatazama barabara ambazo zimejengwa na *TARURA*. Vijiji vyote tunaona *TARURA* imeweza kujenga barabara za vumbi na barabara za changarawe kuhakikisha kwamba mazao yetu ya biashara na mazao ya chakula yanatoka kwenye upande wa uzalishaji kwenda kwenye soko. Hili ni jambo muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona, Waziri wa Maji amezungumza hapa, Sekta ya Maji tumeona uwekezaji mkubwa wa Serikali. Vyanzo vikubwa vya maji vimetumika katika kupeleka maji na inakwenda kutengenezwa gridi ya Taifa ya maji. Hii inakwenda kutusaidia kupeleka maji vijijini na wananchi waweze kupata maji kwa maana ya matumizi ya ndani, matumizi ya viwanda na matumizi ya umwagiliaji ili tuweze kuongeza uzalishaji na kuweza ku-*boost* uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, upande mwingine ni miundombinu ya TEHAMA. Waziri wa Mawasiliano amezungumza hapa, mkongo wa Taifa umejengwa zaidi ya kilometa 12,000. Pia, tunaona kabisa mawasiliano kwa nchi yetu ni makubwa, mpaka vijijini watu wanapata mawasiliano ya simu, wanapata mawasiliano ya *internet*, na wanalipa fedha kwa kutumia njia ya mtandao. Hii ni moja ya njia ya kusukuma

uchumi wa nchi yetu, kurahisisha *transactions* mbalimbali, na hii inakwenda ku-*boost* uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona uwekezaji mkubwa kwenye usafirishaji. Reli imejengwa, lakini tumeona kabisa kabisa kwamba mambo mengi yamefanyika katika kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu hausimami, uchumi unatembea na kuweza kukuza uchumi ili tutoke tulipokuwa tukizalisha au kupata pato la Taifa la bilioni 85 dola za Kimarekani na tunakwenda kwenye ile Dira mpya ya Mwaka 2050. Tunataka pato la Taifa letu lifikie kiwango cha dola trilioni moja.

Mheshimiwa Spika, niseme, kwa kuwekeza huku katika sekta hizi wezeshi, tutaweza kufika kirahisi hasa kwa kuzingatia kwamba kuna sekta nyingine za uzalishaji na sekta nyingine ambazo tunasema ni *transformative sector* kuhakikisha kwamba tunakwenda kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya fedha, Rais wetu ameweka mazingira mazuri. Tumeona mikopo mingi imetolewa katika Sekta Binafsi kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanawekeza na biashara inafanyika katika kuhakikisha kwamba wananchi wanakuza au wafanyabiashara wanakuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hizi sekta nyingine ambazo tunaziita *transformative sector* kama vile sekta ya kilimo, sekta ya uzalishaji, sekta ya madini, utalii, na Uchumi wa Bluu, tumeona Rais wetu amekuwa makini kuhakikisha kwamba sekta hizi zinawezeshwa na zinakwenda kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sekta ya kilimo tumetambua ni sekta inayoajiri watu wengi. Tuwekeze kwenye kilimo na kwenye kilimo lazima tuzingatie mambo makubwa manne. Lazima tuongeze uzalishaji; cha pili, tuongeze *processing* kwa maana ya kuongeza thamani ya mazao yetu; cha tatu, ni kuhakikisha kwamba tunawekeza katika kuhakikisha kwamba tunafanya *good packaging* na kuweza kuuza *product* zetu au bidhaa zetu nje ya nchi na kuzifanyia *marketing,* na kuziuza hizi bidhaa katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, katika uzalishaji wa mazao mbalimbali na hasa yale ya kimkakati, lazima tuongeze uzalishaji ili tuweze kupata tija katika uzalishaji wa mazao hayo.

Waheshimiwa Wabunge, baadhi wamezungumza akiwemo Mheshimiwa Prof. Muhongo kwamba tuwekeze katika kuhakikisha kwamba tunawekeza katika tafiti. Hata Mheshimiwa Dkt. Kimei amezungumza kwamba tuwekeze kwenye utafiti ili tuwe na maamuzi mazuri katika kuhakikisha kwamba tunaongeza tija au tunafanya maamuzi mazuri katika kuongeza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mawazo haya ya Waheshimiwa Wabunge tunayapokea, ni mawazo mazuri. Tuna haja sasa ya kuwekeza kwenye tafiti mbalimbali ili kusudi tafiti hizo ziweze kusaidia katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine limezungumzwa ni suala la kuhakikisha tunaiandaa jamii vizuri ikiwemo suala la elimu. Amezungumza Mheshimiwa Prof. Muhongo hapa kwamba tunatenga fedha kidogo, kiasi cha shilingi trilioni 2.4 kwa ajili ya suala la elimu.

Mheshimiwa Spika, tuzingatie yale malengo au tuzingatie yale maelekezo ya kutenga asilimia mbili ya pato la Taifa. Tukitenga asilimia mbili ya pato la Taifa, tutakwenda kutenga shilingi trilioni 4.2 kwa sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema na ninahakikisha kwamba Serikali yetu ni sikivu na sisi tuliomo humu tunajua ni namna gani tutakwenda kulitekeleza hilo na tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye sekta ya elimu ili kuwawezesha vijana wa Kitanzania waweze kuwa na ujuzi mbalimbali ili waweze kufanya uzalishaji wenye tija na kuongeza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa Sekta ya Kilimo ninapozungumzia uzalishaji, nichukulie mfano kwenye zao la pamba. Zao la pamba hata sasa wanasiasa wameamua kulichukulia kama ni zao ambalo wanaliingiza kisiasa. Ninaweza nikatoa mfano, wanasiasa wengine

wamekuwa wanapita wanazungumza kwamba Serikali isaidie katika kuongeza bei ya pamba.

Mheshimiwa Spika, tumefanya tafiti za kutosha tukaona kwamba bei siyo tatizo, tatizo ni uzalishaji. Ukienda India, heka moja inayolimwa ya pamba inazalishwa pamba kilo 2,500, ikizalishwa pamba kilo 2,500 huyo mtu akiuza anapata fedha nyingi. Tanzania heka moja kule kwetu Simiyu tunazalisha kilo 150 au mwingine ambaye amefanikiwa sana anazalisha kilo 200 mpaka 300.

Mheshimiwa Spika, ukichukua kilo 200 hata leo bei ninapozungumza sasa hivi bei ni shilingi 1,200.00. Bei ya shilingi 1,200.00 ukisema leo mkulima tununue pamba kwa shilingi 5,000.00 amepata kilo 200 tu katika heka moja, atapata shilingi 1,000,000.00 tu ambayo bado ni fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, tukiongeza uzalishaji, akatoka kuzalisha kilo 200, akazalisha walau kilo 1,000 akauza kwa shilingi 1,200.00. Huyu mtu atapata fedha nyingi sana, shilingi 1,200,000.00. Akiuza kwa shilingi hata 1,000.00 ambayo ni chini ya shilingi 1,200.00 lakini akapata kilo 2,500 kama mtu wa India anavyopata. Atapata shilingi 2,500,000.00.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukaona kwamba uzalishaji ndiyo tatizo. Ninamshukuru sana Rais wetu, kupitia Wizara ya Kilimo wamewekeza sasa hivi katika kuongeza uzalishaji wa zao la pamba na mazao mengine. Wamepeleka maafisa wa *BBT*, wanapeleka mbolea ya ruzuku, wanapeleka mbegu za ruzuku, na wamepeleka matrekta. Hii yote ni kuhakikisha kwamba wanaongeza uzalishaji. Tukishaongeza uzalishaji na tukawekeza vizuri katika Sekta ya Kuchakata, Mtanzania ataweza kuwa na tija katika mazao yake.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, bei ya pamba inakuwa *determined* na Soko la Dunia. Leo ukiingia katika mtandao, Soko la Dunia inaonesha bei ya *limit* kwa siku ya leo. Bei hiyo, tunaishukuru Serikali ilikuwa ikimlinda mkulima; inasimamia bei ya pamba na mkulima anapewa bei elekezi na Serikali kwamba, usiuze pamba chini ya shilingi kadhaa na mwaka huu ilikuwa shilingi 1,150.00.

Mheshimiwa Spika, bei hii imelindwa na Serikali kwa sababu imetazama Soko la Dunia linasemaje. Sasa tusiendelee kutegemea Soko la Dunia katika zao la pamba kwa sababu Soko la Dunia bei ya pamba itakuwa ipo chini. Serikali imekuja na uamuzi mkubwa wa kuwekeza kwenye uzalishaji wa zao la pamba na sasa hivi uwekezaji wa zao la pamba ukiwekezwa ina maana matumizi ya zao la pamba yatakuwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pia, mzalishaji wa pamba akizalisha pamba ataiuza ndani, hatasubiri kwenda kuiuza nje ambapo kule nje wanapanga bei yao. Tukiwekeza kwenye viwanda, zao la pamba litakuwa na mahitaji ya ndani na sasa hivi mkulima atapata tija katika uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kuzungumza hayo, Mheshimiwa Waziri wangu atazungumza mengi. Nichukue fursa hii kuendelea kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Maswa na hasa wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki, wamekuwa na mimi muda wote, nimewatumikia kwa kipindi cha pili.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa Maswa, nimezunguka, nimeongea na wananchi wa Maswa wamesema nimefanya kazi vizuri, hawana haja ya kuweka mtu mwingine, wanakwenda kunichagua kwa mara nyingine ya tatu ili nirudi hapa niweze kulitumikia Taifa langu, na niweze kuwatumikia wananchi wa Maswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue fursa hii, nikuombee sana kwa wananchi wa Uyole waweze kukuchagua. Wewe sio Spika wa Uyole peke yake, wewe ni Spika wa Kimataifa, wewe ni Mbunge wa Kimataifa, wao tunawaomba tu waku-*endorse* kwa niaba yetu. Wewe ni Mbunge wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa ujumbe hapa kwamba pia yupo Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Dkt. Tausi Kida, karibu sana. *(Makofi)*

Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Hamad Chande, kisha mtoa hoja Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ajiandae. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hoja iliyopo Mezani kwetu. Ninakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu Raheem, Mola ambaye kwa uwezo wake na neema yake, bado ametujalia tuwe na rasilimali ya uhai. Rasilimali ya uhai ndiyo peke yake thamani ya mwanadamu. Kwa hiyo, tumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa katika hali ya uzima na afya.

Mheshimiwa Spika, pili, ninaomba kumshukuru sana na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye yeye ndiye mbeba maono ya Watanzania. Kwetu sisi Mheshimiwa Rais ni neema ambayo Mungu ametuletea, na wengi sasa hivi wameanza kuelewa na ambao hawajaelewa wajifunze tu kupitia vitabu vyote vitakatifu waone kwamba Mwenyezi Mungu anaweza kuleta baraka na neema kupitia mtu ambaye ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani yeye ana uwezo mkubwa sana wa kutafsiri sera kwa vitendo. Mara nyingi huku duniani jirani zetu walikuwa wanasema kwamba ukitaka mipango na sera nzuri, basi nenda nchi fulani, lakini kwenye utekelezaji kwa vitendo sasa ilikuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, ila tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sera zilizopo ambazo ameziona, amezikuta na amezitengeneza yeye wakati akiwa ni kiongozi anazitekeleza na kuzitafsiri kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, wote leo ni mashahidi, hakuna hata sekta moja ambayo ipo nyuma katika utekelezaji wa sera hizo kwa vitendo. Mheshimiwa Rais huyu, mimi nasema kwamba, Mama Samia ni fahari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nakupongeza na kukushukuru sana wewe. Umekuwa ni mwalimu mzuri kwetu, umekuwa mkufunzi mzuri kwetu, kwa kweli sisi tunaendelea kujifunza kupitia kwako. Tunakuomba tu usituchoke, endelea kutufunza maana hata sasa hivi hapo uko juu ya kiti, nimeona unatoa darasa kwetu sisi. Tunakushukuru sana, tuwaombe tu wenzetu wa kule Uyole, Mheshimiwa Spika huyu anatosha. Wakati huo Mbeya Mjini wao walichagua Mbunge, lakini alipofika hapa akawa siyo Mbunge tu, akawa ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haikusimama hapo, amekuwa ni Rais wa Mabunge ulimwenguni. Tunakushukuru na kukupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia, ninaomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile naomba nimshukuru na kumpongeza sana Naibu Waziri Mkuu. Viongozi hawa wanaendelea kutupa maelekezo siku hadi siku kwa lengo tu la kujenga Taifa letu, wao wamekuwa ni walimu wazuri kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia, nimshukuru sana *chief whip* wetu, Mheshimiwa Lukuvi. Ama kweli usemi unasema kwamba, isiyo kongwe haivushi, anatusaidia kwa kiasi kikubwa sana na amekuwa ni *reference* yetu. *Chief* wetu, Mheshimiwa Lukuvi, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia, niwapongeze na kuwashukuru sana Mawaziri wote ambao tukonao. Kwa kweli, Waheshimiwa Mawaziri hawa, kwetu sisi Naibu Mawaziri, wamekuwa ni walimu wazuri na wanatuelekeza bila kujali kwamba, huyu anatoka katika sekta yangu, wao wanatuelekeza. Tunashirikiana nao kwa wingi kwa shughuli nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Naibu Mawaziri wenzangu kwa namna tulivyoshirikiana vya kutosha katika ujenzi wa Taifa letu hili. Kipekee, naomba nimshukuru sana Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, yeye ni Daktari kweli, ni daktari wa ukweli, siyo wa bahati mbaya. Nakushukuru sana, umekuwa mwalimu mzuri na mlezi mzuri.

Mheshimiwa Spika, haya yote mnayoona tunafanya na tunaenda vizuri ni kwa sababu ya maelekezo na malezi yake. Tunakushukuru sana na tutakuja kuwashangaa sana Wanairamba siku moja kutafuta mtu mwingine. Maana sisi kule nyumbani tunasema, "sumu ya panya haionjwi." Unaweza ukaonja mchuzi wa mbuzi, kuku, lakini sumu ya panya, haionjwi. Siyo mahali pa kujaribu kutafuta mtu mwingine. Ni mahali pa kusimama hapo hapo, mturejeshee Mheshimiwa Waziri wa Fedha aendelee kuchapa kazi na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Huyu amekuwa ni mwalimu wangu wa karibu sana, yaani hata baadhi ya istilahi na misamiati huwa ananiambia hili fanya hivi, hili sema hivi. Nakushukuru sana Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana pacha mwenzangu, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais. Nakushukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Nyongo kwa ushirikiano wako. Tumekuwa pacha mimi na wewe, ukiwa na kazi kwako unaniita; ikiwa iko kwangu nakwambia naomba hapo nenda kafanye hiyo kazi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli, mimi nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu mkubwa sana. Yaani tangu tumeanza Bunge hili mpaka tumefika hapa, wapo wanaofurahia pengine kumaliza hizi siku, maana tunatambua kwamba, wakati umetaradadi sasa, lakini tupo ambao tuna huzuni maana nyumba uliyoizoea, kuihama ina taabu. Kwa kweli, ushirikiano wetu huu ambao tumekuwanao katika Bunge hili na Waheshimiwa

Wabunge wenzangu kwangu imekuwa ni faraja kubwa sana na kujifunza mengi. Hata yaliyotokea ni kwa sababu ya sala na dua za Waheshimiwa Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia, nimpongeze sana sana Naibu Spika, Mheshimiwa Zungu, na Wenyeviti wako wote. Wamefanya kazi kwa uadilifu mkubwa sana na kwa umahiri wa hali ya juu. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya yote hayo, naomba niende kidogo kwenye hoja, ushauri na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kinachofurahisha kuanzia siku ya mwanzo mpaka leo siku ya saba, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanashauri, wanapendekeza na kutoa maoni. Michango yao ni mikubwa na mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuhakikishia kwamba, michango na ushauri wao umechukuliwa na unaenda kufanyiwa kazi kwa sababu, ulikuwa ni ushauri mzuri sana. Kwa hiyo, kwa sababu walishauri, nami naomba tu niweke angalizo katika ushauri mchache huu ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza, yuko Mbunge, Mheshimiwa Neema, amezungumzia suala la *NGO's* kubadilishiwa utaratibu ama kanuni zilizopo. Kwa kweli, Serikali inatambua umuhimu, inatambua thamani na mchango mkubwa sana unaotolewa na *NGO*. Kwa kweli, mchango wao ni mkubwa sana kwa Taifa letu, hususan kwa shughuli mbalimbali katika sekta zetu tofauti; sekta ya elimu, afya, kilimo, mazingira na nyinginezo. Kwa kweli, wana mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, *NGO* yoyote ambayo itakidhi vigezo, itapata msamaha bila pingamizi lolote. Namtoa shaka kabisa na nimwambie *NGO* hizo ziendelee kufanya kazi na kutoa huduma, kama ambavyo zimejiwekea kwenye malengo yao. Serikali itatoa *support* yake kwao na zitapata msamaha, zile ambazo zimekidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, wako Waheshimiwa Wabunge karibu watatu, wanne wamezungumzia umuhimu wa elimu juu mlipakodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalitambua hili na inakubaliana na mapendekezo hayo kwamba, ni lazima Serikali iendelee kutoa elimu. Serikali inatoa elimu siku hadi siku kupitia vyombo vya habari mbalimbali, kupitia makongamano, kupitia semina na hata shule za sekondari tumeanzisha insha maalum, kwa ajili ya elimu ya ulipaji kodi.

Mheshimiwa Spika, pia elimu ya juu, vyuo vikuu, wako na programu mbalimbali za kupeana elimu juu ya umuhimu wa kulipa kodi. Kwa hiyo, tutaendelea na programu hizo katika sekta mbalimbali, lakini tayari tumekubaliana na Wizara ya Elimu, hili tutahakikisha kwamba, limeingia katika mitaala yetu ya elimu msingi na sekondari, ili watu wajue umuhimu wa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, hivi leo tumeona bajeti yetu hii ambayo tunaenda kuipitisha sasa, kwa asilimia kubwa sana inahitaji mapato ya ndani. Kwa hiyo, mlipakodi ni mimi na wewe. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge katika hili la kutoa elimu tushirikiane kuendelea kutoa elimu, kama ambavyo tumeanza huko nyuma, ili kusudi watu walipe kodi kwa hiari kwa sababu, kodi yetu ndiyo maendeleo yetu.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia leo *SGR,* tunapozungumza Bwawa la Mwalimu Nyerere ni kodi yetu mimi na wewe. Kwa hiyo, natoa wito kwa wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuendelee kulipa kodi kwa hiari bila shuruti, ili kujenga Taifa letu hili.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni wastaafu. Mheshimiwa Janejelly, *staff* mwenzangu, huwa anazungumzia sana wastaafu, hasa ambao wanalipwa na Wizara ya Fedha. Naomba nimhakikishie kwamba, Mheshimiwa Rais amesikia kilio kile, amesikia sauti ile na ameitafsiri kwa vitendo. Zaidi ya 100% Mheshimiwa Rais ameongeza, yaani kutoka shilingi 100,000.00 hadi shilingi 250,000.00 wastaafu hao wanaenda kufaidika hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu, mara zote huwa nasema kwamba, Mheshimiwa Rais uwezo wake mwingine mkubwa sana alionao ni kutafsiri sauti ya kila mmoja au kilio cha mtoto wake kwa vitendo. Wako wengine wanaweza wakatafsiri, lakini wakashindwa kutafsiri kwa vitendo. Mama yeye ana uwezo mkubwa sana wa kutafsiri kilio cha mtoto wake kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilitokea kisa kimoja, nilikuwa nimekaa na *uncle* wangu, mtoto wa miezi miwili tu akaanza kulia. Basi, mama akaja, analia nini?

Mheshimiwa Spika, mama akatafsiri kwamba, huyu anachohitaji hapa sasa hivi ni maji ya kunywa. Akapewa maji, akanyamaza. Alipolia sauti nyingine, mama akatafsiri kwamba, mh, kwa sauti hii sasa huyu anahisi kulala. Akatengenezewa mazingira na akalala kweli; lakini akatoa sauti, akasema kwa sauti hii sasa huyu ana homa au mafua yamembana; basi akapewa dawa, ile *Panadol* na akaendelea kupoa kweli, huyo mtoto.

Mheshimiwa Spika, siku moja sasa, yuko *uncle*, yeye tafsiri yake ilikuwa ni moja tu. Mtoto alipolia, maji ya kunywa. Alipolia tena, maji ya kunywa. Yaani asingetokea mama, huyo mtoto tungempoteza. Tunashukuru mama akatokea na mambo yakaenda vizuri. Huu ndiyo uwezo mkubwa sana wa mama, namna ya kutafsiri sauti kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sauti zote, ukisikiliza sauti ya elimu, miundombinu ya elimu imeimarishwa na ajira za walimu zimeendelea. Sauti iliyotoka kwa afya, miundombinu ya afya imeimarishwa, wataalam wameajiriwa na vifaatiba vimepatikana. Sauti iliyotoka kwa ajili ya miundombinu ya barabara, mama ametafsiri, barabara zimepelekwa. Huyo ndio mama. Tunasema mama ni fahari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba niwashukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha

Mapinduzi. Namshukuru sana kwa imani yake kwangu, namshukuru kwa imani kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wanachama wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi na Waheshimiwa Wabunge kwa kweli, dua na sala zenu Mungu amezipokea. Nami niwaambie tu, wahenga wanasema, "Zimwi likujualo halikuli likakwisha." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wanakojani, Wanajimbo la Kojani, kwa kunileta hapa kuwa Mbunge. Baada ya kufika hapa Mheshimiwa Rais imani yake ikasababisha aniteue kuwa Naibu Waziri wa Fedha, sekta nyeti sana. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nawashukuru sana Viongozi wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Wete, Kaskazini Pemba, mikoa yote miwili. Nawashukuru kwa mapokezi makubwa sana, nadhani uliona mwenyewe. Nawashukuru sana kwa mapokezi yale kwa kweli, wamenitendea haki na wamefurahia nafasi hii ambayo ametupa Mheshimiwa Rais, ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Mwenyezi Mungu atujalie tukifika huko turudi wote, tuje tukutane hapa katika mjengo huu kwa lengo la kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba radhi kwa yeyote ambaye nimemkwaza kwa sababu, wakati mwingine tunajibu maswali, inawezekana nimetumia neno ambalo halikumfurahisha mmoja, wakati mwingine hata kutoka mlangoni huwa tunagongana gongana hivi; kama ile imekukwaza, naomba radhi sana. Tumwombe Mwenyezi Mungu atujalie kila la heri tuweze kurudi tena hapa katika mjengo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru tena wewe pamoja na wasaidizi wako ambao wameongoza mjadala huu, akiwemo Mheshimiwa Mussa Zungu, Naibu Spika; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mwenyekiti wetu wa Bunge; Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mwenyekiti wetu wa Bunge; na Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mwenyekiti wa Bunge. Nawashukuru sana kwa jinsi mjadala huu ambavyo umekwenda kwa siku saba.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru tena Kamati yetu ya Kudumu ya Bajeti, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwa uchambuzi wao makini. Kwa maoni na ushauri wao walioutoa kuhusu tathmini ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/2026, Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na jinsi ambavyo tumeendelea kushirikiana nao. Hata tumefanyanao kikao cha mwisho jana mpaka katikati ya usiku.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote na hususan Waheshimiwa Wabunge 120 ambao wamepata nafasi ya kuchangia. Mwaka huu wamepungua kidogo ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024, Waheshimiwa 137 walichangia, mwaka huu wa 2025, ni 97 ukijumlisha na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wanakuwa 120, lakini mwaka huu wakipungua inaeleweka kwa sababu mambo ndiyo hayo tena. Nawashukuru kwa michango yao mizuri sana.

Mheshimiwa Spika, tumepokea maoni na ushauri uliotolewa. Kama ambavyo Waheshimiwa Naibu Mawaziri wamesema vizuri kwa kweli, mwaka huu, 2025, kwa kiasi kikubwa michango imelenga kuonesha kazi kubwa iliyofanyika. Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya CCM, kwa

ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa, ameonesha mafanikio katika ngazi ya Taifa, lakini muhimu zaidi amebainisha mafanikio katika jimbo lake. Kwa hiyo, nadhani mwaka huu, 2025, imekwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kubainisha wazi, kama nilivyosema, kazi ambazo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imezifanya kupitia mipango na bajeti ambazo Waheshimiwa Wabunge waliziidhinisha hapa.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa michango yao ambapo jana pia, wapo wa sekta wameonesha mambo makubwa, kazi kubwa iliyofanyika na mafanikio yaliyopatikana katika nchi yetu kwa sekta zao. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa kazi yangu hapa siyo kubwa, zaidi ya kuweza kuhitimisha.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, nawashukuru pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wetu wawili, kwa jinsi ambavyo wamejibu baadhi ya hoja. Nawashukuru na kuwapongeza sana, tunafanyanao kazi kwa karibu sana, kama nilivyosema siku ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nyongo ni mtu rahimu sana, mtu mwema, mtu mtulivu sana. Ukiwa na msaidizi kama huyu, unafanya kazi kwa usalama na tunaamini kwamba, wenzetu wa Maswa Mashariki, kama kawaida yao, watamrudisha hapa Bungeni. Hivyo hivyo Mjumbe wetu wa Kamati Kuu, Mheshimiwa Hamad Chande, ni mtu mwema, tunafanyanaye kazi kwa karibu, ana bidii na tunaamini wapiga kura wake, kama alivyosema mwenyewe, watat urudishia naye hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa bajeti nzuri sana aliyoiwasilisha hapa Bungeni, tarehe 12 Juni, mwaka 2025. Bajeti hii kwa ujumla wake imepokelewa vizuri sana, siyo tu na Waheshimiwa Wabunge, lakini pia hata na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia vyombo vya habari. Kwa mfano, hivi ndivyo baadhi ya vyombo vya habari ambavyo viliripoti Bajeti Kuu ya Serikali. Gazeti la Nipashe, liliita hii ni "Bajeti ya Kimkakati," *Daily News* wao waliita *"Competitive and Growth Budget,"* *The Citizen* wakaita *"Made for Tanzania,"* maana yake ni kwamba, ni bajeti inayokwenda kuchochea sekta ya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, pia, Mwananchi, wao waliita Bajeti ya Kimkakati, na Habari Leo, wenyewe walisema "Bajeti Yakonga Mioyo ya Wananchi." Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, bajeti ambayo ameiwasilisha imepokelewa vizuri na Umma wa Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema pia, sisi wote hapa mbele, huku *front bench,* ni Mawaziri na tunafanya kazi kama timu tukitafsiri na kutekeleza maono, maelekezo na miongozo ya Mheshimiwa Rais pamoja na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali ya Serikali tunayoipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu watakubaliana nami, nikimpa pongezi za ziada Waziri mwenzetu wa Fedha kwa sababu, kwa kweli, yeye ndiye hutangaza kodi na kwa asili yake kodi huleta lawama. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekuwa akibeba lawama kupitia kodi anazotangaza kwa niaba ya Serikali na kwa niaba yetu wote. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, Mheshimiwa Dkt. Nchemba amejitahidi sana kufanya kazi yake vizuri. Ndiyo maana leo hii tunajivunia miradi mikubwa iliyotekelezwa, kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, *SGR* na madaraja makubwa. Tusisahau kiwezeshi kikubwa ni fedha, fedha ambazo Mheshimiwa Dkt. Nchemba amezisimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Nchemba kwa kazi nzuri anayoifanya kwa nchi hii kwa miaka hii tangu awe Waziri wa Fedha na kwa uwakilishi wake makini. Sina shaka kwamba,

wananchi wenzangu na ndugu zangu wa Iramba Magharibi watamrudisha Bungeni hapa kwa kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ufafanuzi wa mambo machache kwa sababu, kama nilivyosema kwa kweli, kwa kiasi kikubwa hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa zilikuwa ni kuonesha kazi na mafanikio yaliyokuwa yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, natumia wakati huu kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja chache ambazo ziliibuka hapa, lakini pia, zilizoibuka hata nje ya Bunge hili katika mijadala mbalimbali ambayo imejadili bajeti pamoja na mpango wetu wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo lililojitokeza hapa ni tafsiri ya ukuaji wa uchumi. Baadhi ya wananchi na wachambuzi wamehoji maelezo yetu kuhusu afya ya uchumi wetu, hususan pale tuliposema kwamba, uchumi wetu umeendelea kuwa himilivu katikati ya mdororo wa uchumi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, duniani kote afya ya uchumi jumla hupimwa kwa mambo makubwa mawili. Kwanza, tunaangalia ukuaji wa pato la Taifa; na pili, tunaangalia mfumuko wa bei. Hakuna nchi yoyote, na hakuna mwanauchumi yeyote atakayezungumzia uchumi bila kutaja hivi vigezo viwili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukishakuwa na hivi vitu viwili ndipo tunaangalia sasa ni kwa namna gani ukuaji huu unakwenda kutafsirika katika maisha ya watu. Tunaangalia maendeleo ya watu, afya, elimu na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, tunatumia vigezo ambavyo vinatumika duniani kote, na tunajilinganisha nacho.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mfano, na unapozungumzia maendelea ya ukuaji wa Uchumi, huangalii tu mara moja, unaangalia *trend* kwamba mwenendo ukoje? Ndiyo maana ukisoma kitabu chetu cha Mpango kinazungumzia mwenendo wa hali ya uchumi, unalinganisha mwaka uliopita na leo na unatumia kigezo hicho kuweza ku-*predict* tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mfano, ukiangalia mwenendo wa uchumi duniani, wastani wa ukuaji wa uchumi wa dunia mwaka 2020 ulikuwa -2.7; 2021 (6.6), 2022 (3.6), 2023 (3.5), 2024 (3.3), na unatarajia mwaka kesho ushuke iwe (3.1). Kwa hiyo, utaona wastani wa uchumi wa dunia unavyoyumba; utapanda hapa, utashuka hapa.

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea hizi kubwa tunazozifahamu mwaka 2020 ilikuwa (-4), 2021 (6), 2022 (2.9), 2023 (1.7), 2024 (1.8). Nchi zinazoibukia na zinazoendelea *(emerging countries)* hizi kubwa ambazo zinakuja kama China na nyingine, mwaka 2020 (-1.7), 2021 (7), 2022 (4.1), 2023 (4.7), 2024 (4.3), unaona vilevile jinsi ambavyo unayumba. Nchi za Asia zinazoendelea mwaka 2020 (-0.5), 2021 (7.8), 2022 (4.7), 2023 (6.1), 2024 (5.3). Tazama kwetu sasa, nchi za *SADC*, nchi za Kusini mwa Afrika ambapo sisi tumo, wastani mwaka 2020 (-4.5), 2021 (5.3), 2022 (4), 2023 ukaruka (15.2), 2024 (1.5). Unaweza ukaona jinsi ambavyo wastani wa uchumi hata nchi za Kusini mwa Afrika unavyoyumba.

Mheshimiwa Spika, twende karibu nchi za Afrika Mashariki *(EAC)* ambapo sisi tumo 2020 (-1), hasi hiyo, maana yake ulishuka. 2021 (5.3), 2022 (4), 2023 (5.2), mwaka jana 2024 (1.5). Samahani *SADC* 2023 ilikuwa (3.9) siyo 15; na Nchi za *EAC* mwaka 2023 (5.2). Tanzania kwa miaka mitano mwaka 2020 (4.8), 2021 (4.9), 2022 (4.7), 2023 (5.1), 2024 (5.5).

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni nini? Namba moja, hatujawahi kwenda kwenye hasi, hatujawahi. Pia pamoja na changamoto zote ambazo dunia ilikumba, utaona kwamba sisi tulibaki *fair stable*. Kwa hiyo, ndiyo tunasema, katikati ya mdororo wa uchumi wa dunia uchumi wa Tanzania umebaki kuwa imara, umebaki kuwa stahimilivu. Takwimu zinasema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mfumuko wa bei. Mwaka 2024 dunia nzima ulikuwa 6.7, 2023; mwaka 2024 (5.8). Nchi za *SADC* ambazo sisi tumo, wastani wa mfumuko wa bei 50.3 mwaka 2023; mwaka 2024 (54.6). Nchi za *EAC* wastani mwaka 2023 (15.5), 2024 (23.4).

Mheshimiwa Spika, Tanzania mwaka 2023 mfumuko wa bei ulikuwa 3.8, mwaka 2024 ni 3.1. Kwa miaka 10 mfululizo mfumuko wa bei wa Tanzania umebaki ndani ya wigo kati ya 3.5%. Sasa tukisema haya, tunazungumza tu ukweli wa kitakwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi pamoja na hali hiyo uchumi wetu umeonyesha ustahimilivu wa hali ya juu sana. Katika kipindi cha miaka 20 uchumi wetu umeweza kukua kwa wastani wa 6.2%, *twenty years consecutively*. Lengo letu la muda mrefu kama Taifa, tunataka kuona uchumi wetu unakua angalau kwa asilimia kati ya nane mpaka 10, kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Muhongo, ili uweze kuongeza kasi ya kupunguza umaskini na kuweza kuzalisha ajira, ndilo lengo letu. Ndiyo maana kwenye dira inayokuja tumeweka wazi kwamba, kiwango cha kukua uchumi kiwe ni hicho. Tunataka twende tukuze uchumi zaidi tufikie angalau dola za Kimarekani trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

Mheshimiwa Spika, tunavyosema hivi, hatujivuni wala hatusemi kwamba tumeendelea sana, au safari yetu imeisha, au ghafla uchumi wetu umekuwa mkubwa kuliko wote duniani, hapana. Tunachosema na ambacho taasisi zote za kifedha duniani; Benki ya Dunia, *IMF*, Benki ya Afrika, na kadhalika zinasema ni kwamba, uchumi wetu umeendelea kuwa imara na himilivu katikati ya mdororo na majanga ya kidunia.

Mheshimiwa Spika, hii ni tathmini ya taasisi zinazoheshimika duniani, zinazoheshimika katika tathmini ya hali ya uchumi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekuwa akieleza kila mara hapa juu ya tathmini ya taasisi za kutathmini madeni kama za *Moody's*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya hali hii ni kwamba, uchumi wetu hautegemei sekta moja. Tumefanikiwa sana katika kunyumbulisha uchumi wetu. Uchumi wetu unabebwa na sekta nyingi siyo moja, ikiwemo kilimo, utalii, huduma, viwanda, madini, sekta ya ujenzi, usafirishaji na kadhalika. Tofauti na nchi nyingi sana, ambao wanategemea zao moja. Zao hilo likiyumba, basi uchumi unayumba. Sisi inatusaidia sana hii kuwa na uchumi wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema, siku saba tulizokaa hapa kujadili bajeti hii, tumeonyesha kwa sauti na mifano hatua kubwa tulizopiga katika nyanja mbalimbali katika miaka hii minne.

Mheshimiwa Spika, nilifanya hivyo katika hotuba yangu, alifanya hivyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika hotuba yake, Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia wamefanya hivyo katika michango yao, wakijikita kwenye yale makubwa yaliyofanyika katika majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, vilevile Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri waliochangia jana na leo walisema hivyo pia wakati wanachangia katika bajeti hii. Mimi kama nilivyosema, sikusudii katika hatua hii kurudia ambayo yamekwishasemwa zaidi ya kutoa muhtasari na hitimisho.

Mheshimiwa Spika, nisisahau ile hotuba yako kwa Mheshimiwa Rais wakati unampa tuzo, ilibeba kila kitu. *It was a very comprehensive analysis* ya kile ambacho tumefanya katika miaka minne. Kwa hiyo, katika siku saba hizi tumeonyesha kwa kweli kuwa Serikali ya CCM inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetekeleza wajibu wake katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, tukumbushane kidogo kwamba, kuhusu kazi za Serikali, ili tupimane vizuri ni muhimu tukakumbushana juu ya majukumu ya Serikali. Serikali ni chombo cha kusimamia mambo makubwa matatu. Kwanza, amani, ulinzi, na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ameonyesha hapa kwamba nchi yetu, majeshi yetu, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kuwa imara, vinasimamia suala la ulinzi na usalama na ndiyo maana nchi yetu inaendelea kuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wengine hata wakisikia tu kwamba, nchi yetu ina amani wananuna. Ukweli ni kwamba nchi yetu bado ina amani, nchi yetu bado salama, nchi yetu bado ni tulivu.

Hatutaogopa wala kuona aibu kusema hivyo na ndiyo maana tunaiombea iendelee kudumu katika amani na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli ya pili, Serikali inasimamia haki na sheria. Humu ndipo kuna utawala bora, utawala wa sheria na demokrasia. Tumeendelea kulisisitiza na kulihimiza jambo hili, na Waheshimiwa Mawaziri jana wamelieleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali ni chombo cha kusimamia maendeleo. Maendeleo gani? Mosi, huduma za uchumi. Ndiyo maana tunajenga barabarabа, tunajenga reli, tunajenga viwanja vya ndege, tunaleta umeme; zote hizi ni huduma za uchumi ambazo Serikali ni jukumu lake la msingi. Hapa tumeonyesha katika wakati tofauti jinsi ambavyo Serikali imewekeza katika barabara, reli, umeme, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inashughulikia huduma za jamii kama vile mambo ya elimu, afya, maji na kadhalika. Tumeonyesha hapa jinsi ambavyo jana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Waziri wa Maji na kadhalika, walieleza mambo ambayo tumeyafanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina jukumu la kuweka mazingira wezeshi katika kufanya shughuli za kiuchumi, uzalishaji, uwekezaji, biashara na kadhalika na kadhalika. Majukumu yote haya ukiangalia Serikali tumeyafanya. Tumeonyesha jinsi ambavyo uwekezaji umepiga hatua jinsi ambavyo biashara zinaendelea kufunguka na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejijengea heshima kwa mambo mengi. Ukiacha heshima tuliyojijengea ya kuongoza mapambano ya ukombozi katika Bara ya Afrika, sifa kubwa inayoitambulisha Tanzania kimafanikio, ni mafanikio yetu katika kutoa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, tunasifika duniani kwa kutumia fedha zetu kwa ajili ya kuwekeza katika rasilimali ya kudumu katika mali ya Taifa yenye thamani kuliko zote, ambayo ni watu wake. Rasilimali kubwa

tuliyonayo kama nchi ni watu wetu. Serikali miaka yote imeendelea kuhakikisha kwamba tunawekeza.

Mheshimiwa Spika, tumefanya hivi miaka yote kwa sababu tunatambua kuwa maendeleo ya kweli ya uchumi hayawezekani ikiwa wananchi ni wajinga au wameelemewa na maradhi. Lazima tuendelee kupiga vita ujinga, umasikini pamoja na maradhi. Hii imekuwa ni ajenda yetu ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Serikali hii ya Rais Samia imewekeza katika kutoa Elimu Bila Ada, kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita. Katika kipindi cha miaka minne, Serikali imetumia shilingi 1,308,900,040,500.00. *One point three trillion,* ikiwa imewekeza kwenye kutoa Elimu Bila Ada, elimu ya awali mpaka *form six*. Tafuteni Afrika, ni nchi ngapi zinafanya hivyo?

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia imetumia shilingi 2,760,000,000,000.00 kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Yote hii ni katika kuwekeza katika rasilimali watu. Tumefanya hivi miaka yetu yote. Tumefanya hivi kwa kasi kubwa katika miaka minne hii ambayo imepita. Ndiyo maana Serikali ya Rais Samia pia imeamua kutekeleza Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, na Bajeti Kuu ya mwaka huu tumeainisha maeneo ya kikodi kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kidogo, hili suala la Bima ya Afya kwa Wote lilitamkwa kwa mara ya kwanza mwaka 1993/1994; na ninaomba ninukuu hapa hotuba ya Rais wetu wa Awamu ya Pili mzee wetu Hayati Ali Hassan Mwinyi wakati anafunga Bunge *1995*, aliekeza kwamba, "katika mwaka wa fedha 1993/1994 wananchi walichangia jumla ya shilingi milioni 244.5 katika Afya."

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na malalamiko makubwa sana wakati ule, kwamba haiwezekani wananchi waendelee kuingia gharama katika afya. Kutokana na hilo, Rais wetu wa wakati huo akaamua, uchunguzi sasa unafanya kuona uwezekano wa kuanzisha Mpango wa Bima za Afya kwa wananchi wote ili mpango huu wa wananchi kuchangia uishe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, 1993/1994 Serikali iliamua kuja na Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Imetekelezwa miaka 30 baadaye katika Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2024 Bunge lako hili limepitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Mwaka huu Waziri wa Fedha ameweka vyanzo maalumu kwa ajili ya kuona kwamba Mpango huu wa Bima ya Afya kwa Wote unaanza. Sasa tukisema haya ni mafanikio makubwa, unakataa vipi? Miaka 30 baadaye ndiyo tunatekeleza Bima ya Afya kwa Wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningekuwa kwenye mkutano wa hadhara, ningetamka neno fulani lakini ngoja tuendelee.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hakuna shaka kwamba katika miaka hii minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia, kazi kubwa imefanyika na mafanikio makubwa yamepatikana. Sasa wale ambao hawaoni, ninaomba niyaseme maneno ya Rais wa Awamu ya Pili kama nilivyosema awali, Hayati Ali Hassan Mwinyi katika hotuba yake ya kulivunja Bunge la Sita aliyoitoa tarehe 28 Julai, 1995 baada ya kuwa ameeleza mafanikio ya Serikali yake yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya utawala. Alisema hivi, ninanukuu:

"Waheshimiwa Wabunge, asiyeyaona maendeleo kwa sababu macho ni magonjwa, ategе masikio asikilize haya tunayoyasema."

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ningeweza kusema, asiyeyaona maendeleo kwa sababu macho ni magonjwa, atege masikio asikilize haya tunayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baadhi ya watu kukataa kuona maendeleo katika jamii yetu, haijaanza leo. Mwaka 1995 mzee wetu Ali Hassan Mwinyi aliliona hili, lakini akasema kama macho ni changamoto, tega sikio lako. Muhimu ni kwamba, wananchi walio wengi wanaona na wanaunga mkono kazi inayofanywa na Serikali ya CCM. Hili ndilo jambo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipotoa takwimu juzi, wananchi wangapi wanaunga mkono Serikali hii? Maneno mengi yamezungumzwa kwenye mitandao, lakini unapinga takwimu kwa takwimu. Mimi nimeeleza takwimu, nimeeleza chanzo chake, nikawapa mpaka *link* ipo kaangalie *Afro Barometer Research Survey* ya mwaka 2024 inasema nini kuhusu nchi mbalimbali za Afrika. Ni ukweli kwamba Watanzania walio wengi wanaunga mkono Serikali ya CCM. Huu ni utafiti. Ni utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami nimeshiriki kwenye mambo hayo kwa muda mrefu kidogo. Kwa hiyo, hapa tunazungumzia utafiti. Utafiti hupingwa kwa utafiti, siyo kwa hasira. Utafiti huwezi kuufuta kwa hasira. Lete utafiti mwingine ambao una-*challenge* utafiti uliopo. Kwa sasa utafiti tulionao unaonyesha kwamba, Watanzania wengi; moja, wanaridhishwa na kazi ya Serikali ya CCM; pili, Watanzania walio wengi wanamuunga mkono Rais wao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema siri hapa, kwa sababu nimeshiriki kwenye tafiti hizi kuelekea Uchaguzi Mkuu. Chama cha Mapinduzi hakiingii kwenye uchaguzi bila utafiti. Tumefanya utafiti, hali ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapokwenda kuhitimisha, niseme kwamba maendeleo ni mapambano ambayo hayana mwisho. Maendeleo ni mchakato endelevu. Hakuna nchi yoyote itafika mahali sisi tumemaliza kuendelea, tuachie hapa, hakuna. Kila nchi inapambana kuendelea, ni mchakato endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato huu tutapata mafanikio na matatizo. Katika mchakato huu yapo mambo tutapatia, yapo mambo hatutapatia. Ndiyo imekuwa hivyo na ndivyo ilivyo duniani kote. Muhimu katika mchakato wa maendeleo ni kujua tunataka kwenda wapi na namna ya kufika tunapotaka kwenda.

Mheshimiwa Spika, katika uongozi wake wa miaka ishirini na nne; utanisamehe ninapenda kumnukuu Mwalimu Nyerere kwa sababu ni mwanzilishi wa Taifa letu. Mwalimu Nyerere alifanya mengi makubwa.

Hata hivyo, yapo mambo alikosea na akayasahihisha, ikiwemo kufuta vyama vya ushirika na kufuta Serikali za Mitaa. Baadaye yeye mwenyewe alijuta na akayasahihisha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya mwisho Bungeni, wakati anaaga rasmi kama Rais, alihitimisha kwa kueleza mafanikio yake makubwa na matatizo aliyokuwa ameyaacha kwa mrithi anayekuja. Alisema, "Kazi kubwa niliyoazimia kuifanya ni kazi ya kujenga Taifa lenye umoja kwa msingi wa heshima na usawa wa binadamu."

Mheshimiwa Spika, tunalo Taifa moja lenye umoja ambalo msingi wake ni heshima na usawa wa binadamu. Unaweza ukasahau yote aliyoyafanya Mwalimu Nyerere ukakumbuka hilo, kwamba tunalo Taifa lenye umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa uungwana wake hakuishia hapo alisema: "Mafanikio yetu ni makubwa sana na hasa wananchi wetu sasa wanatembea kwa heshima na kujiamini na wana haki kujivunia kuwa Watanzania." Pamoja na mafanikio haya Mwalimu Nyerere hakusita wala kuona aibu kueleza matatizo aliyokuwa ameyaacha alisema: "Hali ya uchumi wetu bado ni mbaya na itabaki kuwa mbaya kwa muda mrefu" akaendelea: "Tunadaiwa madeni makubwa sana na mashirika ya Kimataifa na hii ndiyo kazi ninamwachia mrithi wangu."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nchi hii tunapoeleza mafanikio yetu hapa hatufanyi hivyo kwa kujidai au kwa kusema sisi tu wajuzi sana wa kuleta maendeleo, tunafanya hivyo kuonesha juhudi na jitihada ambazo tumezifanya na mafanikio tuliyoyapata. Tunafanya hivyo kuonesha kwamba katika safari yetu ya maendeleo tumepiga hatua kubwa, lakini tunatambua kwamba bado safari ni ndefu na ndiyo maana tunaendelea kupambana.

Mheshimiwa Spika, Waasisi wa Taifa hili walitufundisha kuwa umuhimu sana kwa kiongozi ni ujasiri wa kubaini changamoto za wananchi na kuzishughulikia lakini pia uungwana wa kubaini na kukiri

makosa na kuyasahihisha kwa wakati muafaka. Hiyo ndiyo nchi ambayo tumerithishwa nayo viongozi wetu wote.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wakienda kusoma hotuba zao zote hususan za mwisho wameainisha mafanikio mazuri na kuonesha changamoto ambazo zimebaki lazima zishughulikiwe. Kwa hiyo, ujasiri wa kukiri makosa na kuyafanyia kazi haijawahi kuwa udhaifu katika nchi yetu na ujasiri huo unahitaji kiongozi makini. Lazima tuwe na kiongozi mwenye ujasiri wa kubaini kutambua, kubeba na kuendeleza mema yote yaliyopita na yanayoendelea ni jambo la msingi sana. Lazima utambue mema yaliyopo, yanayoendelea na uyabebe huo ni ujasiri, lakini pia kukubali kubeba changamoto zimelizoibuka ili uweze kuzishughulikia. Tunahitaji kiongozi mwenye ujasiri wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, sisi tuna bahati tunaye kiongozi ambaye mosi, aliweza kubaini mambo makubwa mazuri yaliyofanyika na mema yote akayabeba na akayaendeleza na wote tumesema hapa katika wiki hii. Vilevile, tunaye kiongozi ambaye ni jasiri, hakuogopa kubainisha changamoto zilizokuwepo katika awamu iliyopita anazibaini, akaziainisha, akaweka mpango wa kuzishughulikia na ndiyo msingi wa *4R*. Kwa hiyo, ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujasiri pia unahitaji chama makini cha siasa chenye uwezo wa kutoa mwelekeo sahihi wa kisera kwa wakati sahihi na unaokidhi mahitaji ya kizazi cha leo na cha kesho na kwa sasa chama hicho kinaitwa Chama Cha Mapinduzi. Niseme nini tena? Twendeni kwa ujasiri majimboni tukaombe Watanzania wachague kiongozi mwenye ujasiri nilioueleza, kiongozi huyo kwa sasa ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Mheshimiwa Spika, kiongozi huyu amefanya kazi kubwa anaelewa nchi inatakiwa kupelekwa wapi anao mpango makini wa kutupeleka huko, juzi *cabinet* imeidhinisha Dira ya Taifa ya Mwaka 2050 na kwa kibali chako tutaiweka Mezani hapa Bunge hili kabla halijaisha. Tunao mwelekeo, tunayo dira ya kutuongoza, tunaye kiongozi makini, kiongozi jasiri ambaye atatupeleka mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twendeni kwa ujasiri majimboni Waheshimiwa Wabunge tukawaombe Watanzania wachague chama makini chenye uwezo wa kutoa na kusimamia mwelekeo sahihi wa kisera kwa nchi yetu, chama hicho ni Chama Cha Mapinduzi. Niwatakie kila la kheri tuombeane afya njema ya kimwili, ya kiroho lakini pia afya njema ya kisiasa majimboni mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nihitimishe kwa shukrani kuitumikia nchi yetu na wananchi katika nafasi ya uongozi kama huu tulionao sisi Mawaziri na sisi Waheshimiwa Wabunge, ni heshima ambayo hakuna yoyote hapa anaweza kusema alistahili. Tumepata heshima kubwa kutoka kwa wananchi wa nchi hii kukaa hapa miaka mitano kutafakari mustakabali wao, ni heshima kubwa ambayo tunaishukuru sana ambayo wananchi wetu wametupa na siyo kwamba tulikuwa tunastahili sana tumepata heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani na heshima aliyonipa kutumikia Serikali yake kwa nafasi ya Uwaziri. Nimshukuru pia Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ambaye aliniona mapema akaniteua kuwa Katibu Mkuu na baadaye kuwa Waziri; lakini mwaka 2021 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliniona akaniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na baadaye kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Ni heshima ambayo imeweka alama ya kudumu katika maisha yangu yote, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ubungo Jijini Dar es Salaam kwa imani yao na hata kunichagua kuwa Mheshimiwa Mbunge wao. Ni kupitia kura zao ambazo zimenipatia fursa ya kuweza kuonekana katika nchi hii na hata viongozi wetu kuniona na kuniteua katika nafasi mbalimbali za uongozi. Ninawaheshimu na nitawaheshimu daima wananchi wa Jimbo la Ubungo; nitawaheshimu na kukiheshimu daima Chama Cha Mapinduzi ambacho kilinipa nafasi ya kugombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nichukue nafasi hii kuishukuru sana familia yangu yenye mke mmoja na watoto watatu. Ninamshukuru sana mke wangu Ndugu Prosista na vijana wangu watatu kwa jinsi

ambavyo wananipa ushirikiano na kunipa amani. Waheshimiwa Wabunge kufanya hizi kazi unahitaji uwe na amani ya kimwili na kiroho, tunaipata amani hiyo kwa kiasi kutoka kwenye familia zetu. Familia ziheshimiwe sana, ni muhimu sana katika maisha yetu na mimi ninaishukuru sana familia yangu kwa sababu inanipa fursa na amani ya kutumikia nchi hii. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamtukuza Mungu kwa yote, tutasema yote hapa ambayo tunayasema hapa na kufanya yote, lakini hakuna tuliwezalo bila Mungu. Hata kuonekana kwetu na hata viongozi wetu wakatuona ni neema tu ambayo tumeipata. Sisi kuwepo hapa katika nafasi hizi siyo kwamba ni wajanja sana au tu wajuzi sana, Hapana, ni kwa neema tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uniruhusu ninukuu tena maneno Matakatifu kutoka kwenye Biblia niliyoyasoma siku ile kwenye mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi pale *Jakaya Kikwete Conventional Centre* nao ni Muhubiri 9:11 yanayosema: "Nitarudi na kuona chini ya jua ya kwamba si wenye mbio washindao katika michezo, wala si walio hodari washindao vitani, wala si wenye hekima wapatao chakula, wala si watu wa ufahamu wapatao mali, wala wenye ustadi wapatao upendeleo lakini wakati na bahati wapata wote." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vyeo hivi bahati mbaya wakati mwingine huja na kiburi tusisahau kwamba sisi hatupo hapa kwa sababu ni wa maana sana isipokuwa wakati na bahati vilikuwa ni vya kwetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninakushukuru tena kwa fursa uliyonipa ya kuhitimisha hoja yangu. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhitimisha hoja. Nikianza na kumshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki kikamilifu Mkutano wa Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao unaelekea kufikia tamati wiki hii. Pia, ninapenda kuona shukrani za dhati kwako mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wako wa Bunge, katika kipindi chote ambacho mmeliongoza Bunge wakati wa majadiliano ya Hoja ya Serikali niliyoiwasilisha tarehe 12 Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kukiri kuwa ni kweli kama nilivyobainisha baada ya mimi kumaliza kusoma hotuba ya bajeti kuwa kulikuwa na utofauti kidogo katika hotuba ya *soft copy* pamoja na vitabu, jambo hili tumelifanyia kazi. Kwa hiyo, hali hii ilitokana na maboresho kidogo ambayo tuliyafanya kwa kuwa kitabu tayari kimekwishachapwa. Hivyo, kwa kuzingatia maboresho hayo ninaomba nakala tepe iliyowasilishwa Bungeni iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge kwa kuwa ilikuwa imezingatia maboresho hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nimewasilisha nakala ngumu 10 za kitabu cha hotuba ya mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliyoboreshwa kwa kuzingatia kwa ajili ya rejea na kumbukumbu. Hivyo, niliombe Bunge lako ile nakala tepe niliyoiwasilisha Bungeni iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutambua kazi kubwa inayofanywa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia na kutoa maoni muhimu hivyo kuwezesha maboresho ya

taarifa hizi. Aidha, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri waliotoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliozungumza na wale waliochangia kwa maandishi. Nitumie fursa hii pia kumpongeza kipekee na kumshukuru ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo. Profesa kweli yeye ni mwalimu kweli yeye ni Profesa tumefanya naye kazi kwa ukaribu sana na hiyo imekuwa chachu ya kurahisisha utendaji kazi mimi kama Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yangu ya Wizara ya Fedha lakini pamoja na timu ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji. Profesa hongera sana na tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema siku ninawasilisha Hotuba ya Serikali tunawaomba wananchi wa Ubungo wamchague tena, wamrudishe kwa sababu bado tunamhitaji aendelee kutoa mchango wako kwa Taifa hili. Amefanya kazi kubwa, mbali na uandishi wa Dira pamoja na Mpango, lakini pia tumekuwa tukishirikiana kwa ukaribu katika hatua za utekelezaji wa miradi kama ambavyo unajua miradi inaanzia kwanza kwenye mipango kabla haijaenda kwenye kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mjumbe wa Kamati Kuu Mheshimiwa Chande kama ambavyo nilisema wakati ule amekuwa Naibu Waziri wa mfano, na wa viwango vya Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha ina vikao ambavyo vinapangwa kabla ya vikao vingine, kwa hiyo kuna wakati tunakuwa kwenye vikao hivyo vya majira ya kipupwe pamoja na mikutano mikuu ambavyo vingine vinaingiliana na Shughuli za Kibunge.

Mheshimiwa Spika, mara zote ninapokuwa kwenye vikao hivyo ninamkuta Naibu Waziri Mheshimiwa Chande ametekeleza majukumu kwa niaba na amefanya kikamilifu na tena bila kuleta mzozo kwenye Kamati na hivyo kuleta ufanisi na kufanya ufanisi wa Wizara uweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri wa upande wa Mipango na Uwekezaji amefanya kazi nzuri, kazi yake ni nzuri. Naibu Mawaziri hawa walikuwa wanatumika kama Wizara bado moja vile, kuna wakati tunamwazima Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mipango na Uwekezaji anasaidia kwenye shughuli za Wizara ya Fedha na kuna wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha anasaidia kwenye shughuli za mipango na uwekezaji, hiyo yote ilikuwa ni katika ushirikiano na wameshirikiana vizuri sana. Tuwaombe Wananchi wa Kojani pamoja na ndugu zangu za Maswa waturudishie tena Waheshimiwa Naibu Mawaziri hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitamalizia mwishoni kwa kuwaomba Wananchi wa Tanzania wawachague tena Waheshimiwa Wabunge hawa wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu kazi ambayo Waheshimiwa Wabunge hawa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameifanya ni kazi ya kutukuta.

Mheshimiwa Spika, niseme mambo machache na yale ambayo yanahusisha hatua za kikodi, tutatolea ufafanuzi kwa sababu bado tuna mjadala wa *Finance Bill* ambao panapo majaliwa tutawasilisha kesho. Kwa hiyo, kuna hoja ambazo tumeendelea kuwa na majadiliano na Kamati pale tutakapokuwa tumemaliza, hata jana tumemaliza takribani saa sita usiku na leo baada ya shughuli hii tutakuwa na kikao, kwa hiyo, majibu yake tutayatoa baada ya kuwa tumeshaweka uelewa wa pamoja na mashauriano ya pamoja na Kamati.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kulitangazia Taifa kwamba nchi yetu ilikuwa kwenye *grey list* nchi zile zinazoangaliwa kwenye masuala ya utakatishaji wa fedha. Nitumie Bunge lako Tukufu kulitangazia Taifa kwamba mwezi huu (wiki iliyopita) nchi yetu imeondolewa kwenye nchi ambazo zipo kwenye *grey list* ambazo zilikuwa katika uangalizi kwenye masuala hayo ya utakatishaji wa fedha. Hii ni hatua kubwa, ni hatua yenye heshima kwa Taifa letu ni hatua kubwa na imetokana na uongozi bora wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambao ameendelea kufanya kwenye masuala ya *good governance*, fedha na kwenye masuala ya uendeshaji wa Serikali unaozingatia masuala ya kitaasisi.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, katika wiki iliyopita Kampuni ya *credit rating* ya *fitch* imeweza tena kuihakikishia Tanzania kwa chapisho lake kwamba imepata *B+*. Utakumbuka kampuni hii ilifanya *credit rating* iliendesha zoezi kwa mwaka jana na mwaka juzi. Mwaka huu imeendesha na imeendelea kusisitizia kwamba Tanzania ina *B+* na uchumi ambao una matazamio ya uimara. Waziri wa Mipango na Uwekezaji ametoka kuelezea uimara huo. Niliona nilielezee hili chapisho mpya ambalo limetoka wiki iliyopita ambalo limeendelea kusisitiza kile ambacho Mheshimiwa Waziri wa Mipango ametoka kukielezea hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja ambazo zilikuwa zimejitokeza ambazo ningetamani kuzielezea hoja ya kwanza ambayo ilijitokeza ni hoja inayohusu Deni la Serikali. Ninaomba nielezee jambo hili kwa utaratibu kufuatana na mijadala ambayo imekuwa ikijitokeza. Suala la Deni la Serikali na ninaomba wananchi kwenye hili tusikilizane vizuri na Waheshimiwa Wabunge. Moja, kuna hoja mbili hoja ya kwanza ni Deni ya Taifa na Deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa ni deni lile linalohusisha Deni la Serikali pamoja na deni la sekta binafsi yote ndani pamoja na nje, kwamba kama kuna mfanyabiashara amekopa kwenye taasisi za kifedha, ameongoza mtaji, amewekeza linapoandikishwa linakuwepo kwenye Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, si kila wakati panapokuwepo na kukua kwa Deni la Taifa ni tafsiri mbaya, kwa sababu kwa utaratibu wa uendeshaji wa kiuchumi kama mtakuwa na makampuni ambayo hayana mitaji yanaendesha utaratibu wa kibiashara kwa taratibu hizi zisizo rasmi, siyo jambo la kujivunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata tunapokwenda kujadiliana masuala ya kifedha, tunapokwenda kujadiliana na *IMF*, tunapokwenda kujdiliana na Benki ya Dunia, tunapojadiliana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunajadiliana sehemu ya fedha zinakwenda kwenye shughuli za Serikali na sehemu ya fedha zinakwenda kwenye taasisi binafsi ili kuwezesha kampuni hizi ziweze kupata mitaji, ziweze kuendeleza uwekezaji na huu ni utaratibu wa kawaida duniani kote.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza hilo ni kwamba wananchi hawapaswi kushtuka hii habari ya Deni la Taifa, Deni la Taifa, Deni la Taifa kwa sababu sehemu kubwa inaenda kwenye upande wa kampuni binafsi na wala si Serikali inayowajibika kulipa na wala si Serikali inayoweka *guarantee*. Wanakopa kwa utaratibu binafsi na wanalipa kwa utaratibu binafsi.

Mheshimiwa Spika, ukirudi kwa upande wa Deni la Serikali. Utaratibu wa masuala ya madeni, ndiyo maana linaitwa Deni la Serikali, hili ni deni linaloangaliwa kwa kuhusianisha na mapato ya Serikali. Serikali zinatumia utaratibu wa kukopa ili ziharakishe utekelezaji wa miradi. Kinachotofautisha Tanzania na nchi zingine ni nidhamu ya matumizi ya fedha hizo zilizokopwa. Kuna nchi na hapa tuelewane vizuri na Watanzania wote, ni kweli kuna nchi zinaingia kwenye matatizo ya madeni na zinaingia kwenye matatizo ya madeni kwa sababu ya kukosa nidhamu ya matumizi ya fedha walizozikopa.

Mheshimiwa Spika, zipo nchi za aina hiyo, wala tusibishane zipo, zinaingia kwenye mitego hiyo ya madeni. Moja, zinakopa bila kuangalia uhimilivu wa kitaalam. Uhimilivu wa kitaalam unazingatia mapato *vis-a-vis* mikopo unayochukua, hii hata kwa mtu binafsi ipo, suala la nidhamu lipo. Jambo la pili ni matumizi ya mikopo hiyo inayochukuliwa. Kwa hiyo, ninawaomba mtu yeyote akitaka tujadiliane suala la madeni, tusijadiliane *figure*, tusijadiliane ile namba, tujadiliane kama kuliwa na umuhimu wa kuikopa hiyo fedha kuhusiana na shughuli tuliyoitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii waende wakaangalie kwenye miradi na mateso ambayo wananchi walikuwa wanapata halafu leo tujadiliane kama ile fedha tuliyoikopa, tulistahili kukopa au hatukustahili kukopa. Kwa mfano, tukienda kwenye deni ambalo lipo upande wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Tumechukua mkopo tumejenga barabara inayotoka Dodoma kwenda Manyara. Zamani kutoka Dodoma kwenda Arusha ilikuwa lazima upitie Morogoro ndiyo uende Arusha.

Mheshimiwa Spika, tuulizane tu, je, ilikuwa ni sahihi kuchukua fedha hiyo tukajenga hii barabara inayokwenda Babati au

tungeacha vilevile deni liendelee kuwa dogo, lakini ukitoka Dodoma ukitaka kwenda Arusha upitie Morogoro na Tanga. Hivyo ndiyo vitu tunavyotakiwa kufafanisha, tusifananishe namba tu kwamba deni limekuwa deni limekuwa, deni limekuwa, kwa sababu deni ni fedha zetu, deni ni fedha ndiyo maana tunahusianisha deni na mapato ya Serikali, ni fedha zetu. Kwa hiyo, ni suala la kuchagua.

Mheshimiwa Spika, haya barabara ya kutoka Singida mpaka Mijingu ni mkopo, ni suala la kuamua sasa tuseme. Kwa waliokuwa wanatoka Singida kwenda Arusha, ukitoka saa tatu Singida unafika saa tatu usiku Arusha na mkiwa abiria, mkiwa na mazao, vyovyote vile lazima mkwame, *then* tukubaliane, je, ulikuwa uamuzi sahihi kuchukua fedha hiyo na kujenga barabara ili uchumi utakaochochewa kutokana na barabara uweze kulipa deni lile? Haya ndiyo mambo tunatakiwa tuyalinganishe, tusihangaike kulinganisha namba kwamba mwaka huu deni lilikuwa hili na mwaka huu deni liko hivi. Tulinganishe kama miradi ile tulikuwa tunaihitaji au hatukuwa tunaihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimejengwa kwa mkopo, fedha zetu za Mifuko. Tunatakiwa tulinganishe, leo tuna wanafunzi wote wale wako Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tuangalie, je, tungebakiza deni liwe dogo tusiwe na chuo hiki, tuendelee kuchagua wanafunzi wachache, waende vyuo vikuu au hivi ambavyo wanafunzi wengi wameweza kwenda kusoma kwenye vyuo vikuu. Hivyo hivyo, hii nimetaja miradi michache tu, tuna miradi mingine mingi ambayo imejengwa kwa utaratibu wa aina hii.

Mheshimiwa Spika, hata hapa kutoka Iringa kuja Dodoma ilikuwa lazima upite Morogoro ndiyo uende Iringa. Hatupaswi kuulizana kuhusu fedha iliyotumika, kuhusu deni lililoongezeka kutokana na fedha tuliyotumia kujenga. Tuulizane kama Je, tulikuwa tunahitaji barabara hii au tungebakiza deni libaki dogo lakini tuwe tunazunguka kutokea Dodoma unaenda Morogoro kwanza ndiyo uende Iringa.

Mheshimiwa Spika, ipo mingi hata Mkongo wa Taifa, *data* hizi tunazotumia, bomba la gesi ni mkopo. Je, tunatakiwa tuulizane kama tungehitaji tuendelee kubakia kianalojia au twende kidigitali halafu tuchachue uchumi. Sasa hivi tunasema uchumi kila kitu ni digitali,

tulitakiwa tuambizane, tuongee kwa takwimu za aina hiyo. Hiyo ni sehemu tu nimetaja, lakini miradi ya aina hiyo iko mingi, tunayo miradi kwenye nishati, tunayo miradi kwenye afya, tunayo miradi kwenye maeneo ya elimu. Huu ni utaratibu wa kutumia mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nalisisitiza hili kwa sababu asiyejua mambo haya huwa wanaenda kuwatisha watoto wa Kitanzania kwamba hata wewe uliye mdogo unadaiwa hiki. Hili ni jambo la mapato ya Serikali na hicho ndicho ambacho huwa tunapima kwenye uchumi. Kwa maana gani ninasema ni mapato ya Serikali, mtu mwingine anasema kama ni mapato sasa si ni Watanzania watalipa? Ndiyo ni matumizi ya mapato ya Serikali kwamba hata bila deni kodi lazima ikusanywe ili kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inaamua kwamba badala nitumie makusanyo ya kila mwezi kumlipa mkandarasi kwenye mradi ambao ukitumia makusanyo ya kila mwezi utaujenga kwa miaka 50, unaamua kwamba nikope muda huu ili mkandarasi amalize mradi na aondoke, halafu yale mapato yangu ambayo ningeyatumia kwenye mradi uleule nitumie kurejesha na yale mapato ni mapato ya Serikali. Ndiyo maana tunapima kwa kutumia vigezo vya mapato ya Serikali. Huo ndiyo uhimilivu tunaouongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema siku ile kwamba hata katika maisha ya kawaida, mtu akishakuwa na chanzo cha mapato kinachoaminika anakipeleka chanzo kile cha mapato ili aweze kupewa mkopo. Anakadiria yale mapato yake kwamba, kama kwa mwezi mapato yake ni shilingi laki tano anaweza kuyavuta yale mapato ya laki tano tano kwa miaka mitano akayaleta hapa leo, halafu anakuwa na kiwango kikubwa kinachoweza kutekeleza jambo kubwa kwa wakati ule. Yale mapato kwa sababu yapo yanakuja, *anyway* angeyatumia tu hata bila kuyakopea, angeyatumia, anatumia kuyalipa kwenye mkopo ilihali akiwa ameshamaliza jambo lake.

Mheshimiwa Spika, fedha tulizokopa tukajenga *UDOM* tungeamua tuanze kujenga msingi kwa makusanyo ya mwezi mmoja, tuje hatua ya pili, tofali la tatu na la nne, tujenge darasa moja, tujenge na la pili, tujenge na la tatu, ingetuchukua miaka mingi, miaka hii

ambayo tunatumia kupeleka marejesho kumaliza kujenga ujenzi ule. Hivyo hivyo na reli, kuna miradi mingine iliyo mikubwa hata huwezi ukatekeleza tu kwa utaratibu ule.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mradi wa dola bilioni kumi kama wa reli, ukitaka uanze kuujenga kwa kukusanya kila mwezi umlipe mkandarasi mpaka ufikishe dola bilioni 10, trilioni zaidi ya 27 maana yake utamweka mkandarasi *site* kwa zaidi ya miaka 40. Hiki ndicho tunachosema kwamba haya ni mapato ya Serikali na wataalam wetu na si wataalam wetu tu, ni wataalam wa Benki ya Dunia, *IMF*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, wataalam hawa *Moody's Fitch Rating,* hawa ambao tumetoka kuwataja, wanaridhika na utaratibu ambao Tanzania inatumia wa kusimamia masuala haya ya mikopo. Ndiyo maana tunasema zaidi ya 73%, 74% ni mikopo ya muda mrefu na ni kwa nini ni mikopo ya muda mrefu, kwa sababu riba zake ni ndogo, lakini pia inatusaidia kupata fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaomba Watanzania, moja, ni lazima tuheshimu hivi vigezo vinavyotumika kupima uhimilivu wa deni la Serikali kwa sababu huo ndiyo utaratibu wa kitaalam. Tunaangalia mapato ya Serikali na yale mapato ndiyo tunatumia kwenye miradi ya maendeleo, kwa hiyo, tunachagua kupata fedha nyingi ili tutekeleze mradi unaotakiwa kukamilika na mapato yale yataendelea kutekeleza mradi husika ili uweze kukamilika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa yule anayetaka mjadala huu asilinganishe namba peke yake, tulinganishe miradi na tuseme kama miradi ile kama ilikuwa inatakiwa. Tanzania haikopi fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hatujawahi kukopa fedha ili tulipe mishahara, hatujawahi kukopa fedha ili tuendeshee magari, hatujawahi kukopa fedha ili tulipe posho. Tunakopa fedha na kuanzia mjadala unapoongelewa, kuanzia mjadala unapoongelewa, unaongelewa kwa mradi mahsusi, fedha inapotoka inakwenda kwenye mradi mahsusi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ndiyo kabisa imezingatia sana kuhakikisha kwamba tunakopa mikopo ya masharti

nafuu ambayo haitaleta mzigo kwenye mapato ya Serikali. Kwa mfano, tumechukua mkopo ule ambao umejenga madarasa yote yale. Tumewaondoa wananchi kwenye kukimbizana huyu na jogoo, huyu mbuzi, wengine wanakimbia, tumewaondoa wananchi kwenye *second selection*. Hii ni hatua kubwa ambayo watoto wanajua wakishafanya mtihani wanajua wanakwenda kwenye masomo.

Mheshimiwa Spika, vimenunuliwa vifaa vya afya, haya ni mambo ya afya. Kwenye nchi ambayo ilikuwa na *CT scan* sijui tatu, sijui nne, leo zimeenda kila mkoa. Hili ni jambo la afya ya Mtanzania! Kwenye nchi ambayo kulikuwa na *MRA* sijui mbili, sijui moja, wapi, eneo la Dar es Salaam peke yake, leo kila Hospitali ya Kanda, Hospitali zetu za Rufaa kote kule mikoani, tumekuwa na jambo hilo muhimu kabisa kwa ajili ya afya za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, si hiyo tu, miundombinu ya maji kila mkoa umepata mtambo wake wa kuchimba maji, miradi ya sekta za uzalishaji, tunawekeza kwenye sekta za uzalishaji, hii ndiyo inayotupa uhakika kwamba tunakokwenda hatuwezi kuelemewa na madeni kwa sababu tunawekeza kwenye miundombinu, tunawekeza kwenye sekta za uzalishaji, tunawekeza kwenye huduma za jamii, tunawekeza kwenye masuala ambayo yanachachua uchumi. Kwa hiyo, niliona niliongelee hili kwa sababu wengine wanapotosha kwa makusudi, lakini wengine kwa kutoelewa kwamba haya ni mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, niseme lingine zuri, tunapojadiliana miradi hii ambayo inahusisha mikopo, tunajadiliana kwa sababu ni maswali yanakuwa yameulizwa, lakini si kwamba Tanzania miradi yote tunayotekeleza ni ya mikopo, si kwamba miradi tunayotekeleza yote ni ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, juzi tumezindua daraja la kisasa ambalo kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki na wa *SADC* hakuna mradi wa aina hiyo umejengwa katika siku za hivi karibuni. Fedha zilizojenga mradi huo ni fedha, ni nguvu ya Watanzania. Ni mradi mkubwa maana yake Tanzania tunaweza kujenga miradi kwa fedha zetu na tunapotekeleza mradi ambao unahitaji uharaka ndiyo tunatumia njia hizo ambazo nimezisema.

Mheshimiwa Spika, tumekamilisha ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, tumetumia fedha zetu. Ni mradi mkubwa na wenyewe tumeweza kutekeleza unaoonesha kwamba nchi yetu ina uchumi unaoweza kusimama na ukaweza kutekeleza jambo kubwa la manufaa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo kubwa ambalo Tanzania imefanya na tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, ni muhimu haya mambo yawekwe sawa ili watu wasiwe wanachanganya.

Mheshimiwa Spika, tumeenda kwenye utaratibu wetu wa vipimo, tumeviangalia vyote kama nilivyotoka kusema na *indications* zake zote kama nilivyosema wakati wa kuwasilisha bajeti. Tulisema jinsi ambavyo takwimu za kitaalam zinaonesha na jambo hilo ni dhahiri na taasisi zote zinazopima masuala ya madeni zimesema hivyo.

Mheshimiwa Spika, sisi tunalo *file* la kuanzia mkopo wa kwanza uliokopwa mwaka 1963, ulienda kwenye shughuli ya maendeleo na Serikali zote zimeendelea na utaratibu huo, tunayo hiyo orodha. Tanzania inaendelea kuwa na heshima ya fedha zake zinazotokana na mikopo kwenda kwenye miradi ya maendeleo. Kwenye *file* hilo tuna miradi takribani 1,112, hiyo ni namba kubwa ambayo inahusisha orodha ya miradi na ni kwa ajili ya muda tu siwezi nikauelezea mradi mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Spika, kinachofanyika ni mradi kuanzia wa kwanza na sekta iliyoenda. Huo ndiyo umekuwa utaratibu wa kujadiliana fedha ya mkopo kwa aina ya mradi ambao unaenda kutekelezwa. Tumetaja miradi mbalimbali, lakini hata iliyo mipya ipo kama ya Msalato, Dodoma hizi barabara za nje, tunayo masuala ya reli, ni fedha ambazo zimejadiliwa na zinakwenda mahsusi kwenye mradi husika.

Mheshimiwa Spika, nikihama kwenye hoja hiyo, kuna hoja ambazo zilijitokeza kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ambazo tumezipokea kwa ajili ya masuala ya kuongeza fedha kwenye utafiti, kuongeza fedha kwenye masuala ya elimu, haya mambo yalielezewa vizuri jana na Waziri wa sekta kwa ajili ya kuokoa muda nitaomba

nikubaliane na maelezo ambayo yalitolewa na Mawaziri wa Kisekta, kwa sababu tayari tulikuwa tumeshakubaliana kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wabunge, zinazohusisha fedha pamoja na miradi inayoendelea. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge pamoja na kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi, lakini fedha za miradi ambayo Wabunge waliomba zitaendelea kwenda kutekeleza miradi hiyo waliyoomba, kwa kuwa nao watakuwepo huko wataendelea kuiona miradi hiyo ikitekelezwa. Miradi hiyo ambayo waliiomba na ndiyo maana tumepitisha bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha ambazo wameziomba kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitaendelea kwenda kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo. Miradi ya maendeleo waliyoiomba itapata fedha na hii iliyokuwa inaendelea kutekelezwa itapata fedha ili iweze kwenda kutekelezwa kwa sababu ni miradi ambayo Serikali imezingatia umuhimu wake na hilo ndilo ambalo limekuwa lengo mahsusi la kutekeleza hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu tumezingatia masuala ya ukuaji wa uchumi ndiyo maana katika baadhi ya maeneo tumeangalia kuweka unafuu ili kuweza kuongeza uzalishaji. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaendelea kukua. Tumeangalia kwenye masuala ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara - MKUMBI, maeneo ambayo yalikuwa yanahitaji Serikali iyafanyie utaratibu ili iweze kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, tunaenda kutekeleza na tumekuwa na rekodi hiyo ya kutekeleza. Fedha ambazo zimekwenda kwenye sekta ya afya zinaashiria Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa Serikali ya aina gani katika masuala ya utekelezaji wa huduma za jamii. Hivyo hivyo kwenye elimu, ametoka kusema Waziri wa Mipango, fedha zilizokwenda kwenye elimu bila ada, fedha zilizokwenda kwenye mikopo ya elimu ya juu, fedha zinazokwenda kwenye miradi hii mikubwa ya kimkakati na hivi tunavyoongea fedha kwa ajili ya

kipande cha tano kinachokwenda Mwanza zimeshakuja, fedha ambazo zitatumika kwa ajili ya kipande cha sita zimeshakuja.

Mheshimiwa Spika, fedha ambazo zitatumika kipande cha saba zimeshakuja na tunakamilisha fedha za kipande cha tatu na cha nne, maana yake Tanzania itakuwa imekamilisha ujenzi wa reli kuanzia Dar es Salaam na matawi yake. Tawi linalokwenda upande wa Kigoma na baadaye kwenda Burundi na *DRC,* lakini na tawi linalokwenda upande wa Mwanza, fedha zake kwa vipande hivyo nilivyovitaja tayari tumeshapata na tutaenda kwenye utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatua kubwa ambayo itaendelea kuionyesha Tanzania ni nchi ya aina gani hasa inapokuja masuala ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tumepokea maoni kwenye upande ule wa zile hoja zilizotolewa kama hoja za kikodi na tutaenda kuzijibu tutakapokuwa tunatoa hoja ya *Finance Bill*.

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nilisema wakati ninatoa hoja hapa na hii iingie kwenye kumbukumbu kwamba Rais wetu ameonyesha umahiri wake na umahiri wa nahodha huwa unapimwa wakati wa msukosuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu ameivusha nchi katika kipindi ambacho nchi zote duniani zilikuwa kwenye misukosuko. Hili ni jambo kubwa liingie kwenye kumbukumbu kwamba Rais wetu ameonesha ushupavu huo na majanga ya dunia hii kwa majira haya yamekuwa ya mfululizo. Zamani tulikuwa tunaona vipindi vikubwa na tunaandikia ma-*thesis* kwamba ilitokea sijui *drought* mwaka fulani inapita miaka 10 ndiyo inatokea *drought* ya aina hiyo. Sijui *oil crisis* ilitokea inapita miaka 10 ama 20 ndiyo inatokea ya aina hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki ambacho Rais wetu ameivusha nchi yetu kumekuwepo na majanga ya mfululizo. Ilikuwa *Covid,* tukiwa bado tunamaliza *Covid* ikaja ya mzozo wa Mashariki mwa Ulaya, tukiwa bado tunamaliza hayo yakaja mabadiliko ya sera za masuala

ya kifedha (uhaba wa fedha za kigeni), tukiwa bado tunamaliza hayo yamekuja mabadiliko ya sera za mataifa marafiki ambayo yanahusu mataifa yanayoendelea ya Afrika kuhusu masuala ya sera za kifedha na sera za kikodi ambayo yote hayo yamekuwa na madhara. Hata hivyo, tukiwa tunamalizia hayo yamejitokeza na mengine ambayo yanaendelea upande wa Mashariki ya Kati, lakini pamoja na hayo yote Rais wetu amesimama kidete na nchi yetu haijayumba kisiasa, kiuchumi, wala kidiplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo kubwa ambalo limeonesha uthabiti wa kiongozi ambaye tunaye kama Watanzania. Tumechukua hatua ambazo zingine zilikuwa za kifedha na zingine za kisera; haijaja hivi hivi na nilielezea wakati ule. Tulichukua hatua ya kutoa ruzuku kwa ajili ya mafuta yanayoingia hapa nchini, tulichukua hatua za kikodi kwa ajili ya bidhaa muhimu ili kuweza kuhakikisha zinaendelea kuwa *affordable* kwa wananchi wetu wa Tanzania na tulitoa fedha kwa ajili ya ruzuku ya mbolea ili Watanzania waendeleze uzalishaji vile vile licha ya masuala yanayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ya mafuta ilipanda; nchi nyingine walianza kupimiana mafuta kwamba kwenye gari A hutakiwi kuweka kiasi fulani cha mafuta na ukishaweka hutakiwi kurudi tena kuweka mafuta ndani ya siku kadhaa, lakini Tanzania tuliendelea kama vile hakuna tatizo lililojitokeza. Hii ni hatua ambayo inatakiwa iendelee kueleweka kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hilo tu, masuala ya kiuchumi Waziri wa Mipango ametoka kuyaelezea. Si nchi zote zimeendelea kuwa na *macros* za aina hiyo na takwimu hizi zinaonekana pia kwenye maisha ya Watanzania. Hii yote ni jambo ambalo limefanyika na ushupavu wa Rais wetu umeendelea kuonekana yanapokuja masuala ya uongozi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoelekea kwenye uchaguzi, CCM imemchagua Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Emmanuel Nchimbi kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi. Hata hivyo, haijawachagua tu wale, imekamilisha Ilani ambayo inaelezea mambo mazuri ambayo Tanzania inaenda kuyapata katika awamu

inayofuata. Si hapo tu, imekamilisha Dira ambapo ndiko mipango ya muda mfupi mfupi (mwaka mmoja mmoja na miaka mitano itakayotokea).

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo tofauti ya Chama Cha Mapinduzi na vyama vingine vyote. Ni chama ambacho kinapanga mambo ambayo kinataka kuwafanyia Watanzania, kinaweka wazi na wenyewe wanapima kwamba hili tunalihitaji. Kimeelezea *transformation* itakayofanyika kwenye sekta za uzalishaji, kimeelezea kazi iliyosalia kwamba kama umeme umeshafika kila kijiji, inayofuata ni kila kitongoji na kila kaya. Kama asilimia imeshafikiwa hii kwenye maji inayofuata ni kumtua mama ndoo kichwani kwenda kwenye kila kaya ipate maji.

Mheshimiwa Spika, Chama kimeelezea kwenye elimu kutoka kwenye elimu tuliyokuwa tunapata kwenda kwenye elimu ya amali na kwenda kwenye elimu ya ujuzi ili mtoto wa Kitanzania aweze kupata elimu ya aina hiyo. Pia, Chama kimeelezea hivyo hivyo kwenye miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema tunaenda kwenye uchaguzi tukiwa na Wagombea wa Urais pamoja na mgombea mwenza ambao hatubahatishi, tuna uhakika nao. Kazi yao tunaijua na tunajua utendaji wao, tunajua *vision* yao na tunajua *patriotism* yao kwa Taifa letu. Tunaenda kwenye uchaguzi tukiwa na chama chenye Ilani ambayo inajulikana na Watanzania hivyo wanaenda kuchagua mambo wanayotaka Serikali iyafanye. Niliona niyaseme haya kwa sababu tunaelekea mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, niendelee kuwapongeza Watanzania kwamba hata sasa tunapoelekea kuhitimisha ngwe ya sasa, Watanzania walichagua Wabunge makini. Leo hii kila sekta wanayoielezea kufanikiwa, taja sekta yoyote kwa taratibu za kibunge, sekta hiyo ilikuwa na Kamati ya Bunge inayofanya nayo kazi. Sisi tulikuwa na Kamati ya Bajeti pamoja na *PIC*, wenzetu wa miundombinu walikuwa na Kamati zao za Miundombinu, wa huduma za jamii walikuwa na Kamati zao za Huduma za Jamii na kazi imefanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania walichagua Wabunge makini. Wakati tunaingia hapa Bungeni ilikuwepo minong'ono kwamba Wabunge hawa wengi itaonekana ni chama kimoja. Sisi tulioko Serikalini ndiyo tunaweza tukasema ilikuwa tunajipanga sana tunapokwenda kukutana na Kamati ya Bunge na tulikuwa tunajipanga sana tunapoleta hoja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uliona mwenyewe moto ulivyokuwa unawaka. Wabunge hawa uchama na urafiki tulikuwa tunakutana nao tukitoka kwenye shughuli za kazi tukienda kwenye *Bonanza* ndiyo tunakuwa marafiki. Kwenye Kamati palikuwa panawaka na Bungeni palikuwa panawaka.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Watanzania na wala wasipate shida kuwarudisha tena Wabunge hawa, wamesimamia Fedha ambazo Dkt. Samia Suluhu Hassan alipeleka majimboni. Miradi ile wanayoiona imefanikiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka majimboni, lakini Wabunge hawa wamefuatilia kuanzia hapa Bungeni na wamefuatilia kule kwenye miradi iliyokuwa inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Bunge hili hili ambalo Watanzania walichagua limepata Spika wewe hapo na umekuwa Rais wa Mabunge yote Duniani. Hii inaonyesha ni namna gani Watanzania walichagua Bunge makini sana. Ni Bunge hili hili lina Waziri Mkuu Majaliwa wameona kazi ambayo amefanya, ni Bunge hili hili lina Naibu Spika pamoja na wale Wenyeviti, ni Bunge hili hili lina Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko na wameona kazi ambazo Wabunge hawa waliowaleta na baadaye wakapata kazi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kazi waliyofanya. Pia, ni Bunge hili hili lina Mawaziri wote hawa na kazi hizi ambazo Mheshimiwa Rais alimwamini kila mmoja na wameona kazi ambavyo imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Wabunge wote hapa amesema vizuri kaka yangu na kwa sababu ni kaka yangu ambalo ameshalisema mimi ninaendelea kupigia mstari tu kwamba hata sisi tuliopata fursa ya kukaa hapa ilikuwa ni dhamana tu angeweza kuwa Mbunge yeyote hapa na angeweza kufanya kazi nzuri hiyo. Hii ni ishara kwamba

Watanzania walichagua Bunge makini, Wabunge makini na ambao wameweza kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaweza nikakupa mifano michache tu nikiwa ninahitimisha. Unaona Wabunge ambao kuna muda walikuwa *back bencher* na baadaye wameingia Serikalini umeona kazi walivyochapa. Hiyo inaashiria ni aina gani Watanzania walileta Wabunge hapa. Kwa hawa waliokuja angeweza kuwa Mbunge yeyote hapa, wamekuja na kazi imeonekana.

Mheshimiwa Spika, ninaweza nikataja wachache; Mheshimiwa Jerry Silaa wameona kazi yake anayofanya, alikuwa kiongozi wa Kamati, alikuwa kwenye Kamati; kwa hiyo, angeweza kuwa Mbunge yeyote. Hii inaonesha jinsi Bunge hili lilivyokuwa na Wabunge makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deus Sangu alikuwa Mwenyekiti wa Kamati na Mjumbe wa Kamati, ameingia Serikalini wameona kazi aliyoifanya; Mheshimiwa Zainab Katimba alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Judith Kapinga alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Daniel Sillo alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Cosato Chumi alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Dennis Londo alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Alexander Mnyeti pia alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Dunstan Kitandula alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Stanslaus Nyongo alikuwa kwenye Kamati ameingia wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa David Kihenzile alikuwa kwenye Kamati ameingia Serikalini wameona kazi aliyofanya; Mheshimiwa Hamad Chande pamoja na Mheshimiwa Dkt. Kiruswa walikuwa kwenye Kamati wameingia wameona kazi waliyofanya. Hii ina maana gani? Watanzania walichagua Wabunge makini na yeyote akiingia alikuwa anafanya kazi na hicho ndiyo kipimo cha kazi wanazoendelea kuzifanya kule kwenye Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa ninamalizia hii hata tusikae kimya, kesho kuna *derby*. Ninawatangazia tu hiyo *boss* wangu atakapokuja keshokutwa atatoa matokeo na hiyo haina kipengele. Tunawatakia kila la kheri watakapokwenda kesho na mambo yote yako vizuri. Kwa hiyo, kesho tunawatakia kila la kheri na sitaki kuweka maneno mengi kwenye hilo, lakini ninaamini itakuwa ni jambo jema sana kwa sababu limesubiriwa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Iramba kwani wamekuwa nami hata katika muda ambapo nimekuwa niko katika kufanya majukumu haya. Ninawashukuru na niwahakikishie kwamba baada ya kumaliza haya majukumu nitaenda kuungana nao na wao walishaniambia ni kwamba mpaka nitembelee mkongojo na mimi bado nina nguvu, kwa hiyo nitaendelea kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia familia yangu ambao juzi walikuwepo hapa (mama pamoja na watoto wote). Ninawashukuru sana kwa kuwa nasi katika maombi pamoja na kuniunga mkono ninapokuwa kwenye haya majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuendelea kuhitimisha nichukue fursa hii pia kuwashukuru taasisi zote za kifedha ambazo tumefanya nao kazi kwa ukaribu sana. Taasisi za kifedha pamoja na nchi washirika wa maendeleo wa Tanzania tunatambua mchango wao niliutaja kwa kirefu lakini tunatambua mchango wao.

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia taasisi zote za ndani ya nchi pamoja na mihimili mingine ikiwemo na Mhimili wa Bunge, Mhimili wa Mahakama na mhimili mzima wa upande wa sheria kwani kila tulipokuwa tuna jambo letu walitusaidia sana. Ninapopongeza mhimili huu niutaje kwa upekee Mheshimiwa *Attorney General* (Mwanasheria Mkuu wa Serikali) amekuwa msaada mkubwa sana katika sisi kufanikisha masuala haya ya kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine Mwanasheria Mkuu kwa jinsi ambavyo tunaenda naye kwenye kazi huwa ninaanza kuona kwamba yeye ni Mwanasheria, lakini pia ni mchumi kwa jinsi

anavyoyaelewa haraka masuala haya na umuhimu wake na amekuwa msaada sana. Tumshukuru pia *Chief Secretary* amekuwa kiunganishi muhimu katika kutekeleza majukumu haya na niwashukuru wataalam wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kuwa Waziri wa Fedha imetegemea sana ubora wa wataalam ambao ninafanya nao kazi nikianza na Katibu Mkuu Dkt. Natu Mwamba ambaye ni Mwalimu wangu pamoja na Manaibu wake ambao wamefanya kazi nzuri na ni watu wanyenyekevu sana na hata Waheshimiwa Wabunge wanapokutana kwenye Kamati wanatambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimtaje kwa upekee Kamishna Jenerali wa Mapato. Ilikuwa kila nikikaa hapa ninapokea malalamiko kutoka kwa Mbunge, lakini Kamishna Jenerali ameweza kuzielewa falsafa za Mheshimiwa Rais kwani amekusanya mapato na hata hapa Wabunge sijapata manung'uniko ya kila dakika kutoka kwenye majimbo yao. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Gavana wa Benki Kuu pamoja na taasisi zingine zote. Gavana wa Benki Kuu ametusaidia kusimamia masuala ya sera za kifedha pamoja na sera za kiuchumi kwa ujumla ndiyo maana hata leo tumeweza kutaja jinsi ambavyo tumevuka.

Mheshimiwa Spika, nitaje na taasisi nyingine zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha tukiwa na *NBS* pamoja na taasisi nyingine zote ambazo tunafanya nazo kazi kwa ukaribu. Wamekuwa nguzo muhimu sana, ninawashukuru sana na kwa kweli ninawatakia kila la kheri na waendelee kulitumikia na kulipenda Taifa letu kama ambavyo wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya jumla ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka 2025/2026 kama nilivyowasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu tulionao baada ya ninyi kuunga mkono hoja mngehojiwa ili hoja iwe sasa imeamuliwa na Bunge, lakini sasa tunafahamu kwa sababu hoja hizi zote mbili tutapiga kura ya wazi baadaye. Kwa hivyo mlikumbushwa jana na niwakumbushe tena wale ambao wako nje ya hapa wajikute wako hapa majira ambayo tutakubaliana hapa kwamba tunakutana kwa ajili ya kuanza zoezi la kufanya maamuzi kuhusu hoja hii ambayo wameshaiunga mkono.

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kusema muda ambao tutarejea hapa basi nilete tangazo la wageni ambao tuko nao hapa Bungeni. Tunao Wageni 19 (wageni wangu) ambao ni Viongozi wa Taasisi ya *Kingdom of Leadership Network Tanzania* wakiongozwa na Ndugu Shalom Nyaga ambaye ni *Chief of Staff KLNT*; Ndugu Winnie Ngaleson ambaye ni *Coordinator* Dodoma; pamoja na Wakili Erick Kidyalla ambaye ni Wakili. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao Wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha ambapo yupo Dkt. Natu Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Elijah Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Ndugu Yusuph Mwenda ambaye ni Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Hivi anaitwa tu kamishna au kuna kitu kimesahaulika? Kamishna Mkuu ama Kamishna Jenerali? Kamishna Mkuu? Haya jamani, yupo Ndugu Yusuph Mwenda ambaye ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Mgeni wa Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Mheshimiwa Erasto Sima. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mhandisi Mathew Andrea Kundo ambaye ni Naibu Waziri wa Maji, hawa ni Wenyeviti wa Vyama vya Upinzani kutoka Bariadi Mkoani Simiyu. Karibuni sana. Sijaorodheshewa vyama mnavyoongoza, lakini tunawakaribisha sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ambao ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma Ndaki ya Mawasiliano ya Kompyuta na Elimu Angavu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambao ni Viongozi wa Kampuni ya Iyula na *Sky Tv* kutoka Vwawa Mkoani Songwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambao ni Wachezaji wa Mpira wa Kikapu, Wanaume na Wanawake watakaoshiriki Taifa *Cup 2025*. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 134 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni Waombaji wa Kumwombea Rais na Taifa kutoka Nchi Nzima wanaitwa TAKURAWA. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wananchi watatu kutoka Jijini Dodoma. Sijui kama hawa wanajijua wenyewe, wananchi watatu kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wananchi wanne kutoka Nzuguni, Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vile vile wanafunzi watatu kutoka Kisasa, Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Walimu sita na wanafunzi 44 wa Shule ya Msingi *Shepherds* kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana Bungeni tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema leo kwa kawaida Bunge huwa tunarejea saa 11, lakini leo zoezi la kupiga kura litaanza saa 10. Kwa hiyo, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 alasiri leo.

*(Saa 6.2l Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Alasiri)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Kumbe lina watu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**na**

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada Katibu ameshatusomea hoja ambayo tunatakiwa kuifanyia uamuzi sasa na uamuzi huu ni ule ambao kila Mbunge ataitika kwa kadri atakavyokuwa ameitwa jina lake. Kwa hiyo, ninawaomba

Waheshimiwa Wabunge utulivu, ili kila Mbunge aweze kusikia jina lake linapoitwa.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba nianze kusoma majina ya Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mhe. Mussa Azzan Zungu - Ndiyo
Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa - Ndiyo
Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko - Ndiyo
Mhe. Job Yustino Ndugai - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Ndiyo
Mhe. Salma Rashid Kikwete - Ndiyo
Mhe. Najma Murtaza Giga - Ndiyo
Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama - Ndiyo
Mhe. Deodatus Philip Mwanyika - Ndiyo
Mhe. Hamza Saidi Johari - Ndiyo
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika - Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi - Ndiyo
Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi - Ndiyo
Mhe. Jenista Joakim Mhagama - Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene - Ndiyo
Mhe. Innocent Lugha Bashungwa - Ndiyo
Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo - Ndiyo
Mhe. Mohamed Omar Mchengerwa - Ndiyo
Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji - Ndiyo
Mhe. Hussein Mohamed Bashe - Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa - Ndiyo
Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu - Ndiyo
Mhe. Dkt. Stergomena Lawrence Tax - Ndiyo
Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni - Ndiyo
Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro - Ndiyo
Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda - Ndiyo
Mhe. Dkt. Dorothy Onesphoro Gwajima - Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana - Ndiyo

Mhe. Jumaa Hamidu Aweso - Ndiyo
Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo - Ndiyo
Mhe. Abdallah Hamis Ulega - Ndiyo
Mhe. Antony Peter Mavunde - Ndiyo
Mhe. Jerry William Silaa - Ndiyo
Mhe. Deogratius John Ndejembi - Ndiyo
Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete - Ndiyo
Mhe. Balozi Mahmoud Thabit Kombo - Hakuwepo
Mhe. Daniel Baran Sillo - Ndiyo
Mhe. Dkt. Festo John Dugange - Ndiyo
Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe - Hakuwepo
Mhe. David Ernest Silinde - Ndiyo
Mhe. Khamis Hamza Khamis - Ndiyo
Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga - Ndiyo
Mhe. Paschal Patrobass Katambi - Ndiyo
Mhe. Eng. Godfrey Kasekenya Msongwe - Ndiyo
Mhe. Hamad Hassan Chande - Ndiyo
Mhe. Dkt. Steven Lemomo Kiruswa - Ndiyo
Mhe. Geophrey Mizengo Pinda - Ndiyo
Mhe. Jumanne Abdallah Sagini - Ndiyo
Mhe. Omari Juma Kipanga - Ndiyo
Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel - Ndiyo
Mhe. Mwanaidi Ali Khamisi - Ndiyo
Mhe. Eng. Maryprisca Winfred Mahundi - Ndiyo
Mhe. David Mwakiposa Kihenzile - Ndiyo
Mhe. Eng. Andrea Mathew Kundo - Ndiyo
Mhe. Judith Salvio Kapinga - Ndiyo
Mhe. Alexander Pastory Mnyeti - Ndiyo
Mhe. Dunstan Luka Kitandula - Ndiyo
Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma - Ndiyo
Mhe. Zainab Athuman Katimba - Ndiyo
Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo - Ndiyo
Mhe. Deus Clement Sangu - Ndiyo
Mhe. Cosato David Chumi - Ndiyo
Mhe. Dennis Lazaro Londo - Ndiyo
Mhe. Fakharia Shomar Khamis - Ndiyo
Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly - Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi - Ndiyo

Mhe. Janejelly James Ntate - Ndiyo
Mhe. Halima James Mdee -Hakuwepo
Mhe. Khalifa Mohammed Issa - *Abstain*
Mhe. Zahor Mohammed Haji - Ndiyo
Mhe. Vita Rashid Kawawa - Ndiyo
Mhe. Ally Juma Makoa - Ndiyo
Mhe. Moshi Selemani Kakoso - Ndiyo
Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza - Ndiyo
Mhe. Jackson Gedion Kiswaga - Ndiyo
Mhe. Fatma Hassan Toufiq - Ndiyo
Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka - Hakuwepo
Mhe. Dkt. David Mathayo David - Ndiyo
Mhe. Timotheo Paul Mnzava - Ndiyo
Mhe. Husna Juma Sekiboko -Ndiyo
Mhe. Oran Manase Njeza - Ndiyo
Mhe. Elibariki Immanuel Kingu - Ndiyo
Mhe. Justin Lazaro Nyamoga - Ndiyo
Mhe. Agustine Vuma Holle - Ndiyo
Mhe. Florent Laurent Kyombo - Ndiyo
Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri - Ndiyo
Mhe. Vincent Paul Mbogo - Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida - Ndiyo
Mhe. Anna Richard Lupembe - Ndiyo
Mhe. Mussa Ramadhani Sima - Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela - Ndiyo
Mhe. Dkt. Thea Medard Ntara - Ndiyo
Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan - Ndiyo
Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga - Ndiyo
Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda - Ndiyo
Mhe. Twaha Ali Mpembenwe - Ndiyo
Mhe. Jafari Wambura Chege - Ndiyo
Mhe. Mary Francis Masanja - Ndiyo

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI**

Mhe. Capt. Abbas Ali Mwinyi - Ndiyo
Mhe. Abdallah Dadi Chikota - Ndiyo
Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo - Ndiyo

Mhe. Abdi Hija Mkasha - Ndiyo
Mhe. Abdul Yussuf Maalim - Ndiyo
Mhe. Abdul-Aziz Mohamed Abood - Ndiyo
Mhe. Abdul-Hafar Idrissa Juma - Ndiyo
Mhe. Abdullah Ali Mwinyi - Ndiyo
Mhe. Abeid Ramadhani Ighondo - Ndiyo
Mhe. Abubakari Damian Asenga - Ndiyo
Mhe. Agnes Elias Hokororo - Ndiyo
Mhe. Agnes Mathew Marwa - Ndiyo
Mhe. Agnesta Lambert Kaiza -Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Ahmed Ally Salum - Ndiyo
Mhe. Ahmed Juma Ngwali - Ndiyo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby - Ndiyo
Mhe. Aida Joseph Khenani - Hakuwepo
Mhe. Aleksia Asia Kamguna - Ndiyo
Mhe. Dkt. Alfred James Kimea - Ndiyo
Mhe. Ali Hassan Omar King - Ndiyo
Mhe. Ali Juma Mohamed - Ndiyo
Mhe. Ali Vuai Khamis - Ndiyo
Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage - Ndiyo
Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila Jumbe - Ndiyo
Mhe. Ally Mohamed Kassinge - Ndiyo
Mhe. Aloyce Andrew Kwezi - Ndiyo
Mhe. Aloyce John Kamamba - Ndiyo
Mhe. Amandus Julius Chinguile - Ndiyo
Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Ndiyo
Mhe. Amina Ali Mzee - Ndiyo
Mhe. Amina Bakar Yussuf - Ndiyo
Mhe. Amina Daud Hassan - Hakuwepo
Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Ndiyo
Mhe. Amour Khamis Mbarouk - Ndiyo
Mhe. Anastazia James Wambura - Ndiyo
Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest - Hakuwepo
Mhe. Angelina Adam Malembeka - Ndiyo
Mhe. Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula - Ndiyo
Mhe. Angellah Jasmine Kairuki - Ndiyo
Mhe. Antipas Zeno Mgungusi - Ndiyo
Mhe. Anton Albert Mwantona - Ndiyo

Mhe. Asha Abdullah Juma - Ndiyo
Mhe. Asia Abdukarimu Halamga - Ndiyo
Mhe. Assa Nelson Makanika - Ndiyo
Mhe. Asya Mwadini Mohammed - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Asya Sharif Omar - Ndiyo
Mhe. Athuman Almas Maige - Ndiyo
Mhe. Atupele Fredy Mwakibete - Ndiyo
Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe - Ndiyo
Mhe. Aziza Sleyum Ally - Ndiyo
Mhe. Bahati Keneth Ndingo - Ndiyo
Mhe. Bahati Khamis Kombo - Ndiyo
Mhe. Bakar Hamad Bakar - Ndiyo
Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa - Ndiyo
Mhe. Benardeta Kasabago Mushashu - Ndiyo
Mhe. Benaya Liuka Kapinga - Ndiyo
Mhe. Boniphace Mwita Getere - Ndiyo
Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo - Ndiyo
Mhe. Boniventura Destery Kiswaga - Ndiyo
Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli - Ndiyo
Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata - Ndiyo
Mhe. Catherine Valentine Magige - Ndiyo
Mhe. Cecil David Mwambe - Ndiyo
Mhe. Cecilia Daniel Paresso - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Charles John Poul Mwijage - Ndiyo
Mhe. Charles Muguta Kajege - Ndiyo
Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei - Ndiyo
Mhe. Dkt. Christina Christopher Mnzava - Ndiyo
Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishangoma - Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka - Ndiyo
Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza - *Abstain*
Mhe. Condester Michael Sichalwe - Ndiyo
Mhe. Constantine John Kanyasu - Ndiyo
Mhe. Daimu Iddi Mpakate - Ndiyo
Mhe. Daniel Awack Tlemai - Ndiyo
Mhe. Deo Kasenyenda Sanga - Ndiyo
Mhe. Dorothy George Kilave - Ndiyo
Mhe. Edward Olelekaita Kisau - Ndiyo
Mhe. Edwin Enosy Swalle - Ndiyo

Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka - Ndiyo
Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai - Ndiyo
Mhe. Emmanuel Peter Cherehani - Ndiyo
Mhe. Eric James Shigongo - Ndiyo
Mhe. Ester Amos Bulaya - Hakuwepo
Mhe. Esther Edwin Malleko - Ndiyo
Mhe. Esther Lukago Midimu - Ndiyo
Mhe. Esther Nicholas Matiko - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa - Ndiyo
Mhe. Felista Deogratius Njau - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Festo Richard Sanga - Ndiyo
Mhe. Flatei Gregory Massay - Ndiyo
Mhe. Dkt. Florence George Samizi - Ndiyo
Mhe. Francis Isack Mtinga - Ndiyo
Mhe. Francis Kumba Ndulane - Ndiyo
Mhe. Fredrick Edward Lowassa - Ndiyo
Mhe. Furaha Ntengo Matondo - Ndiyo
Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe - Ndiyo
Mhe. George Natany Malima - Ndiyo
Mhe. George Ranwell Mwenisongole - Ndiyo
Mhe. Ghati Zephania Chomete - Ndiyo
Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi - Ndiyo
Mhe. Grace Victor Tendega - Ndiyo *(Makofi)*
Mhe. Haji Amour Haji - Ndiyo
Mhe. Haji Makame Mlenge - Ndiyo

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

Mhe. Hamida Mohamed Abdallah

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida si upo hapo?

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

Mhe. Hamida Mohamed Abdallah - Ndiyo
Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla - Ndiyo
Mhe. Hamisi Shabani Taletale - Ndiyo
Mhe. Hasan Seleman Mtenga - Ndiyo

| | |
|---|---|
| Mhe. Hassan Zidadu Kungu | - Hakuwepo |
| Mhe. Hawa Mchafu Chakoma | - Ndiyo |
| Mhe. Hawa Subira Mwaifunga | - Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Hussein Nassor Amar | - Ndiyo |
| Mhe. Iddi Kassim Iddi | - Ndiyo |
| Mhe. Innocent Edward Kalogeris | - Ndiyo |
| Mhe. Innocent Sebba Bilakwate | - Ndiyo |
| Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwelwe | - Ndiyo |
| Mhe. Issa Ally Mchungahela | - Ndiyo |
| Mhe. Issa Jumanne Mtemvu | - Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Kainja Andrea | - Ndiyo |
| Mhe. Jacqueline Ngonyani Msongozi | - Ndiyo |
| Mhe. Jaffar Sanya Jussa | - Ndiyo |
| Mhe. Janeth Elias Mahawanga | - Ndiyo |
| Mhe. Janeth Maurice Massaburi | - Ndiyo |
| Mhe. January Yussuf Makamba | - Ndiyo |
| Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi | - Ndiyo |
| Mhe. Jesca David Kishoa | -Ndiyo *(Makofi)* |
| Mhe. Jesca Jonathani Msambatavangu | - Ndiyo |
| Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo | – Ndiyo |
| Mhe. John Marko Sallu | – Ndiyo |
| Mhe. Jonas Van Zeeland | – Ndiyo |
| Mhe. Jonas William Mbunda | – Ndiyo |
| Mhe. Joseph Anania Tadayo | – Ndiyo |
| Mhe. Joseph George Kakunda | – Ndiyo |
| Mhe. Joseph Kasheku Musukuma | – Ndiyo |
| Mhe. Joseph Michael Mkundi | – Ndiyo |
| Mhe. Joseph Zacharius Kamonga | – Ndiyo |
| Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima | – Hakuwepo |
| Mhe. Josephat Sinkamba Kandege | – Ndiyo |
| Mhe. Josephine Tabitha Chagula | – Ndiyo |
| Mhe. Josephine Johnson Genzabuke | – Ndiyo |
| Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako | – Ndiyo |
| Mhe. Juliana Daniel Shonza | – Ndiyo |
| Mhe. Juliana Didas Masaburi | – Ndiyo |
| Mhe. Juma Hamad Omar | – Ndiyo |
| Mhe. Juma Othman Hija | – Ndiyo |
| Mhe. Juma Usonge Hamad | – Ndiyo |

Mhe. Jumanne Kibera Kishimba – Ndiyo
Mhe. Kabula Enock Shitobelo – Ndiyo
Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni – Ndiyo
Mhe. Kassim Hassan Haji – Ndiyo
Mhe. Katani Ahmadi Katani – Ndiyo
Mhe. Kavejuru Eliadory Felix – Ndiyo
Mhe. Kenneth Ernest Nollo – Ndiyo
Mhe. Khadija Hassan Aboud – Ndiyo
Mhe. Khadija Shaaban Taya – Ndiyo
Mhe. Khalifa Salum Suleiman – Ndiyo
Mhe. Khamis Kassim Ali – Ndiyo
Mhe. Khamis Yussuf Mussa – Ndiyo
Mhe. Kunti Yusuph Majala – Ndiyo
Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo – N diyo
Mhe. Latifa Khamis Juwakali – Ndiyo
Mhe. Leah Jeremiah Komanya – Ndiyo

**SPIKA:** Ngoja, ngoja Katibu

Mhe. Leah Jeremiah Komanya – Ndiyo

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

Mhe. Eng. Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho – Ndiyo
Mhe. Balozi Liberata Rutageruka Mulamula – Ndiyo
Mhe. Livingstone Joseph Lusinde – Ndiyo
Mhe. Lucy John Sabu – Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga – Ndiyo
Mhe. Luhaga Joelson Mpina – Hakuwepo
Mhe. Maida Hamad Abdallah – Ndiyo
Mhe. Maimuna Ahmad Pathan – Ndiyo
Mhe. Maimuna Salum Mtanda – Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta – Ndiyo
Mhe. Mariam Nassoro Kisangi – Ndiyo
Mhe. Mariam Madalu Nyoka – Ndiyo
Mhe. Martha Festo Mariki – Ndiyo
Mhe. Martha Nehemia Gwau – Ndiyo
Mhe. Maryam Azan Mwinyi – Ndiyo

Mhe. Maryam Omar Said – Ndiyo
Mhe. Masache Njelu Kasaka – Ndiyo
Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki – Hakuwepo
Mhe. Maulid Saleh Ali – Ndiyo
Mhe. Mbarouk Juma Khatib – Ndiyo
Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani – Ndiyo
Mhe. Michael Costantino Mwakamo – Ndiyo
Mhe. Michael Mwita Kembaki – Ndiyo
Mhe. Minza Simon Mjika – Ndiyo
Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu – Ndiyo
Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi – Ndiyo
Mhe. Mohamed Lujuo Monni – Ndiyo
Mhe. Mohamed Said Issa – *Abstain*
Mhe. Mohamed Suleiman Omar – Ndiyo
Mhe. Mohammed Maulid Ali – Ndiyo
Mhe. Mrisho Mashaka Gambo – Ndiyo
Mhe. Muharami Shabani Mkenge – Ndiyo
Mhe. Munde Tambwe Abdallah – Ndiyo
Mhe. Munira Mustapha Khatib – Ndiyo
Mhe. Mustafa Mwinyikondo Rajab – Ndiyo
Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge – Ndiyo
Mhe. Mwanakhamis Kassim Said – Ndiyo
Mhe. Mwantakaje Haji Juma – Ndiyo
Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis – Ndiyo
Mhe. Mwantumu Dau Haji – Ndiyo
Mhe. Mwantumu Mzamili Zodo – Ndiyo
Mhe. Mwita Mwikabe Waitara – Ndiyo
Mhe. Nancy Hassan Nyalusi – Ndiyo
Mhe. Nape Moses Nnauye – Ndiyo
Mhe. Nashon William Bidyanguze – Ndiyo
Mhe. Ndaisaba George Ruhoro – Ndiyo
Mhe. Neema Gerald Mwandabila – Ndiyo
Mhe. Neema Kichiki Lugangira – Ndiyo
Mhe. Neema William Mgaya – Ndiyo
Mhe. Ng’wasi Damas Kamani – Ndiyo
Mhe. Nicholaus George Ngassa – Ndiyo
Mhe. Nicodemas Henry Maganga – Hakuwepo
Mhe. Njalu Daudi Silanga – Ndiyo

Mhe. Noah Lemburis Saputu Mollel – Ndiyo
Mhe. Norah Waziri Mzeru – Ndiyo
Mhe. Nusrat Shaaban Hanje – Ndiyo
Mhe. Oliver Daniel Semuguruka – Ndiyo
Mhe. Omar Ali Omar – Abstain
Mhe. Omar Issa Kombo – Ndiyo
Mhe. Omari Mohamed Kigua – Ndiyo
Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo – Ndiyo
Mhe. Prof. Patrick Aloyce Ndakidemi – Ndiyo
Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato – Ndiyo
Mhe. Pauline Philipo Gekul – Ndiyo
Mhe. Philipo Augustino Mulugo – Ndiyo
Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya – Ndiyo
Mhe. Priscus Jacob Tarimo – Ndiyo
Mhe. Rashid Abdallah Shangazi
Mhe. Rashid Abdallah Rashid – Ndiyo
Mhe. Ravia Idarus Faina – Ndiyo

**SPIKA:** Ngoja, ngoja Katibu, subiri.

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Rashid Shangazi alikuwa ameshapiga kura, huyo aliyekuwa anaitwa sasa hivi na Katibu ni Rashid Abdallah Rashid.

Mhe. Rashid Abdallah Rashid – Ndiyo
Mhe. Ravia Idarus Faina – Ndiyo
Mhe. Regina Ndege Qwaray – Ndiyo
Mhe. Rehema Juma Migilla – Ndiyo
Mhe. Dkt. Ritta Enespher Kabati – Ndiyo
Mhe. Robert Chacha Maboto – Ndiyo
Mhe. Rose Cyprian Tweve – Ndiyo
Mhe. Rose Vicent Busiga – Ndiyo
Mhe. Saada Monsour Hussein – Ndiyo
Mhe. Saashisha Elinikyo Mafuwe – Ndiyo
Mhe. Salim Alaudin Hasham – Ndiyo
Mhe. Salim Mussa Omar - Ndiyo
Mhe. Salome Wycliffe Makamba – Ndiyo
Mhe. Salum Mohammed Shaafi – *Abstain*

Mhe. Samweli Xaday Hhayuma – Ndiyo
Mhe. Santiel Eric Kirumba – Ndiyo
Mhe. Sebastian Simon Kapufi – Ndiyo
Mhe. Seif Khamis Said Gulamali – Ndiyo
Mhe. Seif Salim Seif – Ndiyo
Mhe. Selemani Jumanne Zedi – Ndiyo
Mhe. Shabani Omari Shekilindi – Ndiyo
Mhe. Shally Josepha Raymond – Ndiyo
Mhe. Shamsia Azizi Mtamba – Ndiyo
Mhe. Shanif Mansoor Jamal – Ndiyo
Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya – Ndiyo
Mhe. Silyvestry Francis Koka – Ndiyo
Mhe. Simai Hassan Sadiki – Ndiyo
Mhe. Simon Songe Lusengekile – Ndiyo
Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda – Ndiyo
Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo – Ndiyo
Mhe. Soud Mohammed Jumah – Ndiyo

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE**

Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula – Ndiyo
Mhe. Stella Ikupa Alex – Ndiyo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya – Ndiyo
Mhe. Stella Simon Fiyao – Ndiyo
Mhe. Stephen Lujwahuka Byabato – Ndiyo
Mhe. Subira Khamis Mgalu – Ndiyo
Mhe. Suleiman Haroub Suleiman – Ndiyo
Mhe. Suma Ikenda Fyandomo – Ndiyo
Mhe. Sylvia Francis Sigula – Ndiyo
Mhe. Tabasam Hamis Mwagao – Ndiyo
Mhe. Tamima Haji Abass – Ndiyo
Mhe. Tarimba Gulam Abbas – Ndiyo
Mhe. Taska Restituta Mbogo – Ndiyo
Mhe. Tauhida Cassian Gallos – Ndiyo
Mhe. Tecla Mohamedi Ungele – Ndiyo
Mhe. Toufiq Salim Turky – Ndiyo
Mhe. Tumain Bryceso Magessa – Ndiyo
Mhe. Tunza Issa Malapo – Ndiyo

Mhe. Ummy Ally Mwalimu – Ndiyo
Mhe. Ussi Salum Pondeza – Ndiyo
Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo – Ndiyo
Mhe. Venant Daud Protas – Ndiyo
Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Ndiyo
Mhe. Yahaya Omary Massare – Ndiyo
Mhe. Yahya Ali Khamis – Ndiyo
Mhe. Yahya Ally Mhata – Ndiyo
Mhe. Yustina Arcadius Rahhi – Ndiyo
Mhe. Zacharia Paulo Issaay – Ndiyo
Mhe. Zaytun Seif Swai – Ndiyo
Mhe. Zubeida Khamis Shaib – Ndiyo
Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka – Ndiyo
Mhe. Zuena Athumani Bushiri – Ndiyo
Mhe. Zulfa Mmaka Omar – Ndiyo

**SPIKA:** Katibu kabla hujafunga zoezi kuna Wabunge ambao waliitwa wakati wa kupiga kura na walikuwa hawajafika bado, sasa wapewe nafasi hiyo ya kuitwa ili wapige kura.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nimemwona Mheshimiwa Ummy Hamisi Nderiananga.

Mhe. Ummy Hamisi Nderiananga – Ndiyo

**SPIKA:** Kuna Mheshimiwa Amina Daudi Hassan

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE**

Mhe. Amina Daud Hassan – Ndiyo

**SPIKA:** Mwingine Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu

Mhe. Hassan Zidadu Kungu – Ndiyo

**SPIKA:** Ngoja uitwe na Katibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu namba 208 Katibu.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE**

Mhe. Hassan Zidadu Kungu – Ndiyo

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryprisca Mahundi

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE**

Mhe. Maryprisca Mahundi – Ndiyo

**SPIKA:** Wamekwisha, Waheshimiwa Wabunge wote mmepiga kura? Zoezi linafungwa sasa. Kuna Mbunge hajapiga kura? Hakuna; Katibu endelea.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kazi ya kupiga kura imekamilika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu anakwenda kufanya hesabu haraka kidogo kisha atarejea hapa ili niwasomee matokeo, tujue kama bajeti imepita au kuna jambo la ziada. Ahsante sana tuvumilie kidogo dakika chache.

*(Hapa kura zilihesabiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kazi inaanza tutafute viti vya karibu tuketi.

Waheshimiwa Wabunge zoezi la kupiga kura kwa ajili ya kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 chini ya Kanuni ya 126 ya Kanuni za Kudumu za Bunge zoezi hilo limekamilika.

**MATOKEO YA KURA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, idadi ya Wabunge wote Kikatiba ni 393, idadi ya Wabunge waliopo mpaka sasa ni 392 na idadi ya nafasi wazi ni moja; idadi wa Wabunge waliokuwepo Bungeni

ukiondoa Spika ni 378; idadi wa Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni ni 13. Sasa matokeo ya kura ni kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, kura za Hapana hakuna, kwa maana ya sifuri; kura za Ndiyo 373; kura ya hakuamua wale waliosikika wakisema *Abstain* ni tano. Sasa ninatangaza rasmi kwamba Bajeti ya Serikali imepitishwa kwa kura 373 sawa na 98.7%. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge, baada ya zoezi hili kukamilika sasa tunaweza kwenda hatua inayofuata. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 56,490,256,212,000 kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2026, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo *(A Bill for an Act to apply a some of fifty six trillion, four hundred ninety billion, two hundred fifty six million, and two hundred twelve thousand shillings out of the consolidated fund to the service of the year ending on the 30th day of June, 2026 to appropriate the supply granted for that year, to authorize the reallocations of certain appropriation, and to provide for matters connected with those purposes)*

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

***Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2025***
***(The Appropriation Bill, 2025)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha jumla ya shilingi trilioni 56,490,256,212,000 kwa Matumizi ya Serikali kutoka katika Mfuko Mkuu Hazina kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2026, kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka huo, kuruhusu kuhamisha baadhi ya fedha pamoja na mambo yanayohusiana na malengo hayo *(A Bill for an Act to apply a some of fifty six trillion, four hundred ninety billion, two hundred fifty six million, and two hundred twelve thousand shillings out of the consolidated fund to the service of the year ending on the 30th day of June, 2026 to appropriate the supply of granted for that year, to authorize the reallocations of certain appropriation, and to provide for matters connected with these purposes)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa mara ya tatu sasa nitawahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025 *(The Appropriation Bill, 2025)*. Wote mmeafiki ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka 2025*
*(The Appropriation Bill, 2025) Ulipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu huwa unasomwa kwa utaratibu huu kwa maana ya kwamba tukishapitisha bajeti basi Muswada huu unapitishwa kwa hatua zote tatu tukiwa tumekaa hapa ndani kwa sababu kinachozungumza ni kile ambacho tumeshatoka hapa kupitisha. Baada ya kuwahoji mmeafiki, nanyi kuafiki, hivyo nitangaze rasmi kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2025 *(The Appropriation Bill, 2025)* umepitishwa rasmi na Bunge. Kama ilivyo ada Muswada huu sasa atapelekewa Mheshimiwa

Rais ili na yeye aweze kufanya kwa sehemu yake kwa kadri Katiba inavyoelekeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii tumefika mahali ambapo Bunge limeshapitisha Bajeti Kuu ya Serikali, lakini pia Bunge limeshapitisha Sheria ya Fedha ambayo tumeipitisha hapa sasa. Kwa kusema hivyo nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninafahamu kuwa sisi sote tunafahamu kwamba kazi ya kutafuta fedha siyo kazi nyepesi na sisi humu ndani wote tunakuwa na hoja za kuzileta kutoka kwenye majimbo yetu kutoka kwenye maeneo yetu ya uwakilishi, lakini wakati mwingine tunazungumza yale ya kitaifa ambayo hata hivyo huwa yanataka Mheshimiwa Waziri aende huko akazisake. Basi Mheshimiwa Waziri tunakupongeza kwa kazi nzuri na tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa Bunge pia kuweza kupitisha bajeti hii sasa inaashiria pia kukubali kwamba yale ambayo yameletwa na Serikali kwamba yatatekelezwa katika mwaka ujao basi yataweza kutekelezeka. Tunawatakia kila la heri katika utekelezaji, lakini wewe na Naibu Waziri msaidizi wako wa karibu kabisa tunawashukuru sana kwa ushirikiano ambao mmeonesha. Kwa kweli Wabunge huwa wanakuwa na hoja nyingi lakini na ninyi mnazipokea zote na mnazifanyia kazi, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. Ninajua pia chini yenu wako watendaji mbalimbali ambao wanahangaika na hayo mambo ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kutafuta hizo fedha kila mahali zinakopatikana na wenyewe tunawashukuru sana wakiongozwa na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa upande wa yale tunayosema kila siku hapa mapato ya ndani na makusanyo na watu walipe kodi, basi kipekee kabisa nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Kamishna Mkuu wa *TRA* kwa kazi nzuri anayoifanya. Tunaamini kwa hatua ambazo zinaendelea kupigwa basi makusanyo yataendelea kuongezeka kwa kadri yanavyopiga hatua sasa tunaona yanakimbia na tunaamini yataendelea kukimbia. Kwa hiyo na yeye tunamtakia kila heri katika hilo zoezi la kuhakikisha

makusanyo yanaendelea kukua. Wakati huo huo sisi Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi, basi na sisi tuwe mfano mzuri kwenye kulipa kodi ili nchi yetu iweze kupata maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hayo mnafahamu pamoja na kwamba nimemtaja Mheshimiwa Waziri wa Fedha lakini wanafanya kazi kwa karibu sana na Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tunakushukuru pia sana kwa kazi nzuri ambayo unaifanya. Ofisi hii ni mpya lakini mnakimbizana nayo na wakati huu Wabunge hawa wanayo matumaini makubwa baada ya kuanza na umetuambia leo asubuhi hapa kukamilika kwa mchakato wa maandalizi ya Dira ya Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaamini kwamba sasa Wizara hii ama ofisi hii itaweza kufanya kazi vizuri zaidi na kwa mpangilio kwa maana ya kwamba Wabunge pamoja na kwamba tutaendelea kuleta hoja za kutoka Majimboni, lakini Serikali itakuwa tayari ina mipango kwa ajili siyo tu ya majimbo lakini kwa ajili ya maeneo yale ya uwakilishi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba dira hiyo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri tunakupongeza pia kwa kazi nzuri na tunakutakia kila la heri katika utendaji wako. Naibu Waziri pia ambaye ndiyo msaidizi wako mkuu na wewe, tunakushukuru sana kwa kazi nzuri na tunakutakia kila la heri na watendaji walio chini yenu wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Kija, tunawatakia kila la heri katika mipango hiyo ya nchi yetu. Sasa tunajua Dira ikishaletwa hapa Bungeni basi mtaanza miaka mitano, mtaanza mwaka mmoja mmoja tunaamini tutaanza kuona nchi yetu ikipiga hatua ndefu zaidi kuliko zile ambazo tukipiga awali kwa hiyo kila la heri katika hayo yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nanyi safari imekuwa ndefu kidogo nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wabunge wote namna ambavyo mmeshiriki katika zoezi hili tangu tuanze zoezi hili la Bajeti za Kisekta, mmefanya kazi kwenye Kamati mkiongozwa na Wenyeviti wetu na Makamu Wenyeviti wa Kamati hizi, mmefanya kazi hii kwa uadilifu mkubwa sana tunawashukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wale sasa wasaidizi wa hapa mbele kwa sababu mkishafanya kazi kwenye Kamati lazima mje hapa. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Ilala tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ambayo umeifanya, Mheshimiwa Zungu kwa kweli ahsante sana. Vilevile, Wenyeviti: Mheshimiwa Najma Murtaza Giga ninakushukuru sana kwa usaidizi mzuri; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama ahsante sana kwa usaidizi mzuri; lakini pia Mheshimiwa Deodatus Mwanyika ahsante sana kwa usaidizi mzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, shukrani hizi haziwezi kukamilika bila kutaja kwa ujumla upande wa Serikali kwa sababu tunashirikiana nao na shughuli tunazozifanya kwa kweli nyingi ni za kwao. Kwa hiyo, ninawashukuru sana Mawaziri wote, Naibu Mawaziri kwa ushirikiano mkubwa ambao mmeutoa kwenye ngazi ya Kamati wakati wakijadili hoja za kisekta, lakini pia baadaye sasa kwenye Bajeti Kuu. Ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu.

Waheshimiwa Mawaziri mmejibu maswali mengi sana ya Wabunge hapa na wakati mwingine sisi tuliokaa hapa mbele tunatoa nafasi hata zaidi ya yale maswali ambayo yametajwa kikanuni ili tu Waheshimiwa Wabunge hawa wapate nafasi ya kusema yale ambayo wametoka nayo kwa wananchi wanaowakilisha. Nyinyi mmekuwa wavumilivu, tunawashukuru sana sana sana. *(Makofi)*

Kipekee Naibu Mawaziri ninadhani ndiyo wamepewa hii kazi ya kujibu maswali, ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu ambao mmeutoa kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa kusema hivyo basi viranja wa upande wa Serikali humu Bunge, Mheshimiwa *Chief Whip* tunakushukuru sana, Mheshimiwa Lukuvi ahsante sana kwa ushirikiano wako. Mambo yamekuwa yakienda vizuri kwa sababu ya ushirikiano wako mkubwa ambao unatupatia. *(Makofi)*

Naibu Waziri Mkuu pia ahsante sana kwa ushirikiano wako ambao unaendelea kutupa tunakushukuru sana sana sana. Umekuwa msaidizi mzuri kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa kweli hata yeye asipokuwepo basi tunajua wapi pa Kwenda, tunakushukuru sana kwa uvumilivu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa ushirikiano wako ahsante sana sana sana. Wakati mwingine anakuwa amekuja hapa Bungeni ana makabrasha yake ametoa hapo anasoma na bado Wabunge wanaenda hawaangalii hata kama kuna jambo anafanya, lakini ni mvumilivu, kwa hiyo anawavumilia. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushirikiano mkubwa ambao umekuwa nao, lakini pia kwa kuongoza jopo la Serikali hapa Bungeni na kuliwezesha kufanya shughuli zake kwa ukamilifu kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa ambalo ni la wageni wenu. Kwanza kuna wageni 114 wa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray ambao ni wanafunzi 106 na Walimu nane wa Shule ya Awali na Msingi ya *Ignatius* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ambao ni mama mkwe na watoto wake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo nitumie pia fursa hii kumshukuru sana Katibu wetu wa Bunge amefanya kazi kubwa sana kwa kweli yeye pamoja na timu yake yote wamefanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba Kamati zinafanya kazi vizuri, lakini Wabunge taarifa zinaandikwa kwa ustadi kabisa. Tunakushukuru sana Katibu wa Bunge kwa ushirikiano ambao umeutoa mpaka tumefika sehemu nzuri mno. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, ninawashukuru wananchi ambao wamewatuma ninyi, ninaamini wameona uwakilishi wenu. Kwa hiyo, tunawashukuru wananchi kwa kuendelea kufuatilia Bunge lao na ili ujue wananchi wanafuatilia ni pamoja na kuyazungumza yanayotokea humu Bungeni yawe madogo ama makubwa. Kwa hiyo wananchi pia tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa…

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga ninaomba uketi.

Waheshimiwa Wabunge ili jambo lake likae vizuri ni kwamba kura zimeshafungwa na zimeshatangazwa na tulishaenda kwenye jambo lingine la kupitisha Sheria kwa hivyo hatuwezi kurejea kule. Pole sana Mheshimiwa Maganga. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 25 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*